# Nipashe

Jumamosi Septemba 12, 2020 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

ISSN 0856 • Na. 0580336

www.ippmedia.com

MWANGA WA JAMII

www.twitter.com/nipashetz www.facebook.com/nipashetz www.instagram.com/theguardian_newspaper LIKE & FOLLOW US




## Jaji Mark Bomani afariki dunia Dar, kuzikwa Jumatatu shambani kwake

UKURASA 2


KUMBE BURNA BOY, STEFFLON NI MKE NA MUME? Ukurasa 14

JUMAMOSI SEPTEMBA 12, 2020

Nipashe BT

KILLY&CHEED

Wameshindwa pera kwa Ali Kiba, wataweza tufaa la Konde Boy?

WALIPOONDOKA katika lebo ya Kings Music, Wanamuziki Killy na Cheed, walikuwa na mengi ya kujitetea ikiwamo kile walichosisitiza kwamba wao wanafuata ushauri wa wazazi wao.

Wengi walishangaa sababu hiyo, wengine walihoji kwa nini wasanii wote waondoke na sababu iwe moja? Lakini kwa wale waelewa walijua safari hiyo kuna nahodha anawaongoza.

Pamoja na kuacha ghafla katika lebo hiyo iliyowatangaza, Ali Kiba ambaye ndiye kiongozi, hakuwa na maneno mengi badala yake aliwatakia safari njema na kuwashukuru kwa kumtambua kama ndiye aliyewaibua.

Juma hili, wasanii hao waliibuka tena, safari hii walitangaza kujiunga na lebo ya Konde Gang, ambayo bosi wake ni mwanamuziki Harmonize.

Katika ujumbe wa wasanii hao wakati wakijiunga na lebo hiyo, walimshukuru sana Ali Kiba kwa kuwatoa kimuziki, pia wakamsifu Harmonize, kwa kuwakubalia wajiunge katika kundi hilo kubwa.

Harmonize, aliwakaribisha kwa ujumbe wenye nasaha na angalizo makini kwa vijana hao.

" Karibuni Killy na Cheed, silaha yetu ni upendo pamoja na kazi, maana hizo ndiyo haja za wananchi wanaoifanya leo hii Konde Gang Music kuwa ulimwenguni, Konde Gan ni lebo kubwa kwa hiyo acha tufanye".

Killy na Cheed wanakumbushwa kwamba pamoja na furaha ya kujiunga na Konde Gang, lakini wakumbuke kwamba ni lazima wachape kazi na kuacha utoto unaofanywa na watoto pacha.

Huko sasa hakutakuwa na mfumo wao wa 'wawili' kila mmoja atambue umuhimu wake na kazi wanazofanya na si vinginevyo.

Wakitaka kufanikiwa ni lazima waache 'upacha' wao kwani wakiendelea na mtindo huo watajikuta wakikumbuka 'pera' walioacha kula kule kwa Ali Kiba na kukimbilia 'Tufaa' la Harmonize ambalo watashindwa kutafuna.

UKURASA 11

# Kubenea amwaga chozi akiachiwa kwa dhamana

UKURASA 2





Mgombea ubunge wa Jimbo la Ubungo kwa tiketi ya Chama cha ACT- Wazalendo, Saed Kubenea, akifuta machozi wakati akizungumza na waandishi wa habari, baada ya kuachiwa kwa dhamana katika Mahakama ya Wilaya ya Arusha jana. Kubenea anashtakiwa kwa makosa mawili likiwamo la utakatishaji fedha. Kulia ni Wakili wake, Shecky Mfinanga na kushoto ni Mwenyekiti wa chama hicho, Mkoa wa Arusha, Mwahija Chogga. Picha ndogo: Kubenea akitolewa kwenye mahabusu ya mahakama hiyo, baada ya kupata dhamana. **PICHA: GETRUDE MPEZYA**


## YALIYOMO

UKURASA WA 3

**MAALIM SEIF ASHINDA PINGAMIZI, RASMI URAIS**

MGOMBEA urais wa Zanzibar kupitia Chama cha ACT-Wazalendo, Maalim Seif Sharif Hamad, ameshinda pingamizi...


## Mchunguzi TAKUKURU mbaroni tuhuma za rushwa

UKURASA 2



## CCM yajivunia kufanya kampeni za kisayansi

UK. 3





Scan Hapa

Fungua App ya QR Code Reader kisha scan kupakua APP yetu

Google Play App Store

Fursa kwa Wagombea! 2020

VOTE

Gazeti la Nipashe linawapongeza wateule wote waliopitishwa na vyama vyao kugombea ubunge katika majimbo mbalimbali nchini

Je ungependa kukishukuru chama chako ?

Je ungependa kutangaza sera zako kwa wapiga kura ?

Nipashe inatoa nafasi kutangaza sera zako kwa gharama nafuu

Nipashe MWANGA WA JAMII

Wasiliana nasi

Simu: 0686 101335,

Barua pepe: advertise@guardian.co.tz

VOTE

# Mchunguzi TAKUKURU mbaroni tuhuma rushwa

**Na Joseph Mwendapole**

OFISA Uchunguzi Mwandamizi (II) wa Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU) Mkoa wa Kinondoni, Nina Saibul, amekamatwa na taasisi hiyo kwa tuhuma za kuomba na kupokea rushwa ya Sh. milioni 4.9.

Taarifa iliyotolewa jana na TAKUKURU na kutiwa saini na Ofisa Uhusiano wake wa makao makuu, Doreen Kapwani, ilisema ofisa huyo anadaiwa kuomba rushwa hiyo kutoka kwa mfanyabiashara anayejihusisha na shughuli za ujenzi wa nyumba za kupangisha (Real Estate).

Ilisema kama ambavyo imekuwa ikitokea kwa taarifa za watuhumiwa wengine, TAKUKURU Mkoa wa Kinondoni ilipokea taarifa za malalamiko dhidi ya ofisa wake huyo kuomba rushwa ili asiendelee na uchunguzi unaodaiwa kuwa ulikuwa ukiendelea.

Taarifa hiyo ilibainisha kuwa baada ya taarifa hiyo kupokewa uchunguzi wa awali wa kuthibitisha tuhuma hizo ulifanyika na kubaini kuwa upo ukweli wa tuhuma hizo za kuomba hongo, lakini hakukuwa na tuhuma wala jalada lolote la uchunguzi unaoendelea dhidi ya mlalamikaji.

"Baada ya TAKUKURU kujiridhisha na uchunguzi huo wa awali, iliandaa mtego uliowezesha kukamatwa kwa Nina na mumewe, Ramadhani Makoye, wakipokea kiasi hicho cha pesa kilichoombwa na Nina," ilibainishwa katika taarifa hiyo.

Ilisema taasisi hiyo imechukua hatua hiyo ili kuhakikisha inajisafisha dhidi ya watumishi wake wachache wenye tabia ovu zenye kuchafua taasisi hiyo na kwamba uchunguzi wa shauri hilo unakamilishwa ili mtuhumiwa afikishwe mahakamani.

"Kwa niaba ya Mkurugenzi Mkuu wa TAKUKURU, tunawashukuru wananchi na wadau wengine ambao wameendelea kushirikiana na taasisi katika kufanikisha jukumu hili la kuzuia na kupam-

# Kubenea amwaga machozi akiachiwa kwa dhamana

**Na Waandishi Wetu**

MGOMBEA Ubunge wa Kinondoni (ACT-Wazalendo), Saed Kubenea, ameachiwa kwa dhamana baada ya kudhaminiwa kwa Sh. milioni 14.5 mbele ya Hakimu Martha Mahumbuga katika Mahakama ya Hakimu Mkazi Arusha.

Kubenea aliachiwa jana baada ya kudhaminiwa na wadhamini wawili ambao ni Mwenyekiti wa Wilaya wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA) Ephata Nanyaro na Mwenyekiti wa Chama cha ACT-Wazalendo Mkoa wa Arusha, Mwahija Choga.

Hakimu Mahumbuga alisema mshtakiwa ametimiza masharti ya dhamana aliyotakiwa kuyafuata ikiwa ni pamoja na kulipa Sh. milioni 14.5 na kuwa na wadhamini wenye mali isiyohamishika.

"Hivyo, mshitakiwa huyu atakuwa nje kwa dhamana hadi Septemba 21 mwaka huu, kesi hii itakapotajwa tena," alisema.

Kabla ya mshtakiwa kudhaminiwa, Wakili wake, Sheck Mfinanga, akishirikiana na Wakili Alute Munghwa, waliwasilisha mahakamani hapo vielelezo vya dhamana hiyo zikiwamo nakala za malipo ya fedha hizo, barua za utambulisho toka serikali za mtaa za wadhamini wake na kukubaliwa na upande wa mawakili wa serikali.

Septemba 7, mwaka huu, Kubenea alisomewa mashtaka yake na Wakili wa Serikali Innocent Njau mbele ya Hakimu Mahumbuga kwa kuingia nchini kinyume cha kifungu cha 45(1)(i) na (2) cha Sheria ya Uhamiaji Sura ya 54. Ilidaiwa mahakamani huko kuwa Kubenea alikamatwa mpakani Namanga Mkoa wa Arusha Septemba 5, mwaka huu na baada ya kupekuliwa alikutwa na fedha za kigeni.

**AMWAGA MACHOZI**

Nje ya mahakama, Kubenea akizungumza na waandishi wa habari baada ya kuachiwa huku akitokwa na machozi, aliwashukuru wananchi wa Mkoa wa Arusha na waandishi wa habari kwa kufuatilia shauri lake hatua kwa hatua tangu akamatwe Septemba 5, mwaka huu.

Katika hatua nyingine, Chama Cha ACT-Wazalendo kimesema kitaendelea na kampeni za mgombea wake huyo zilizosimama kutokana na kukamatwa na polisi kwa tuhuma za utakatishaji fedha na kuingia nchini kinyume cha sheria.

"Chama cha ACT-Wazalendo kinapenda kuutaraifu umma wa Watanzania na wananchi wa Kinondoni kwamba mgombea wetu wa ubunge, Ndugu Saed Ahmed Kubenea amepata dhamana ya Hakimu Mkazi Arusha leo (jana)," ilielezwa katika taarifa hiyo iliyosisitiza chama hicho kuendelea na kampeni kwenye jimbo hilo.

**Imeandikwa na Cynthia Mwilolezi (ARUSHA) na Enock Charles (DAR)**




Katibu wa Itikadi na Uenezi wa Chama Cha Mapinduzi (CCM), Humphrey Polepole, akizungumza na waandishi wa habari mjini Chato, Mkoa wa Geita, jana. **PICHA: IKULU**

# Jaji Mark Bomani afariki dunia

**Na Mwandishi Wetu**

MWANASHERIA Mkuu wa zamani wa Tanzania, Jaji (mstaafu) Mark Bomani (88), amefariki dunia katika Hospitali ya Taifa ya Muhimbili (MNH) jijini Dar es Salaam.

Jaji Bomani ambaye alikuwa Mtanzania wa kwanza kuwa mwanasheria mkuu na wa pili tangu uhuru, alifariki dunia usiku wa kuamkia jana hospitalini hapo alipokuwa amelazwa kwa siku 24.

"Jaji Mstaafu Bomani amefariki majira ya saa 4:00 usiku na alikuwa hapa hospitalini kwa siku 24," alithibitisha Ofisa Uhusiano wa MNH, Aminiel Aligaesha.

Habari ambazo zilipatikana baadaye zilieleza kuwa nguli huyo wa sheria anatarajiwa kuzikwa Jumatatu shambani kwake, Goba jijini Dar es Salaam.

Bomani aliyekuwa na shahada ya sheria kutoka Chuo Kikuu cha Makerere, Uganda, alikuwa Mwanasheria Mkuu wa Tanzania kuanzia mwaka 1965 hadi mwaka 1976 akichukua nafasi hiyo kutoka kwa Roland Brown. Kabla ya kuwa mwanasheria mkuu, alikuwa Naibu Mwanasheria Mkuu kuanzia mwaka 1962.

Jaji Joseph Warioba alichukua nafasi yake na kudumu nayo mwaka 1976 hadi 1985 alipoteuliwa kuwa Waziri Mkuu na Makamu wa Kwanza wa Rais.

Tangu mwaka 1976 alikuwa mshauri mwandamizi wa sheria wa Umoja wa Mataifa (UN) kuhusu uhuru wa Namibia hadi mwaka 1990.

Pia alikuwa msaidizi wa Rais wa Kwanza wa Tanzania, Mwalimu Julius Nyerere na baadaye Rais wa zamani wa Afrika Kusini, Nelson Mandela, katika usuluhishi wa mgogoro wa Burundi kutokana na vita vya wenyewe kwa wenyewe.

Licha ya nafasi hizo, Jaji Bomani aliwahi kuwa Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi ya Serengeti Breweries Limited. Pia alikuwa akimiliki kampuni ya uwakili ya Bomani and Company Advocates.

Mwaka 1995, Bomani alikuwa mmoja wa wanachama wa Chama Cha Mapinduzi (CCM) waliojitokeza kugombea urais wa Tanzania lakini alienguliwa katika ngazi za awali. Rais (mstaafu) Benjamin Mkapa (sasa marehemu) ndiye aliyeshinda na kuwa mgombea baada ya kumshinda Rais (mstaafu) Jakaya Kikwete katika raundi ya pili ya uchaguzi.

**CCM YAMLILIA**

Chama cha Mapinduzi (CCM), kimeelezea kusikitishwa na kifo cha mwanasheria huyo mkongwe ambaye pia aliwahi kuwa mwanachama wake.

Katibu wa Itikadi na Uenezi wa CCM, Humprey Polepole, akizungumza na waandishi habari wilayani Chato jana, alisema wamepokea kwa masikitiko kifo cha Jaji mstaafu Bomani.

Polepole alisema Jaji Bomani aliitumikia CCM kwa muda mrefu na kugombea nafasi ya kuteuliwa kuwania nafasi ya urais ndani ya chama.

"Jaji Bomani alikuwa mwanachama mwaminifu na mtiifu ndani ya CCM. Pia alidumu kama Mjumbe wa Baraza la Wadhamini ndani ya chama. CCM imepata msiba mkubwa kwa kuondokewa na kada mtiifu. Natoa pole kwa umma wa Watanzania kwa msiba huu," alisema Polepole.



Mgombea urais wa Jamuhuri ya Muungano wa Tanzania, kupitia Chama cha ADC, Queen Sendiga, akizungumza katika ufunguzi wa mkutano wa kampeni za chama hicho, uliofanyika viwanja vya Mnazi Mmoja mjini Zanzibar jana. **PICHA: RAHMA SULEIMAN**

# CCM yajivunia kufanya kampeni za kisayansi

**Na Gwamaka Alipipi,** CHATO

CHAMA Cha Mapinduzi (CCM), kimesema kinajivunia kufanya kampeni zake za uchaguzi mkuu kisayansi, kikitamba kuwa hadi kufikia Oktoba 27, mwaka huu, kitakuwa kimekifikia kila kijiji nchini.

Katibu wa Itikadi na Uenezi wa chama hicho, Humphrey Polepole, aliwaambia waandishi wa habari Chato mkoani Geita jana kuwa CCM kwa sasa inafanya kampeni za kisayansi na weledi wa hali ya juu kwa kujigawa katika makundi yanayoshambulia kila kona ya nchi.

Polepole alikuwa akizungumzia tathmini ya siku 10 za mwanzo za kampeni za chama hicho, akidai kuwa wamebaini endapo uchaguzi mkuu ukifanyika sasa, mgombea urais kupitia chama hicho, Dk. John Magufuli ataibuka mshindi kwa asilimia 85.

Alisema hadi sasa Dk. Magufuli ameshafanya kampeni katika mikoa minane, mgombea mwenza, Samia Suluhu Hassan, ameshafika mikoa ya nyanda za juu, kusini na kati, akitumia usafiri wa barabara na kufanikiwa kufika kila kijiji.

Alisema mjumbe wa kamati kuu, Kassim Majaliwa, Waziri Mkuu, ameshashambulia mikoa ya Dodoma, Manyara na Arusha wakati viongozi wengine akiwamo Rais mstaafu Jakaya Kikwete wakifanya kampeni mikoa ya kusini, huku mjumbe mwingine wa kamati kuu, Mizengo Pinda na Spika Job Ndugai, wakishambulia mikoa ya kanda ya kati.

"Hadi ifikapo Oktoba 27, mwaka huu (siku moja kabla ya uchaguzi), tutakuwa tumefika kila kijiji, kila kata, kila kitongoji, kila mkoa tutakuwa tumefika, tumejigawa na tunashambulia kila kona," alitamba Polepole.

Polepole alisema CCM ina kitengo cha utafiti ambacho kimekuwa kikishirikiana na vitengo vinginevyo na kwamba Februari kiliwahoji wananchi 4,998 na kupata matokeo ya asilimia 90 ya ushindi kwa Dk. Magufuli.

Alisema kuwa katika utafiti wa kisayansi walioufanya, endapo uchaguzi ungefanyika mwezi huu, CCM ingeshinda kwa asilimia 75 upande wa wabunge na asilimia 85 kwa madiwani.

"Tutaimaliza nchi hii awamu hii yote, kisha tutapiga awamu nyingine, na kisha tutapiga awamu nyingine. Kwa sasa tumejiimarisha, wanachama tulionao kwa sasa ni milioni 17," alitamba.

Polepole pia alijibu hoja ya wapinzani wao kisiasa kuhusu serikali kutoongeza mishahara kwa watumishi wa umma, akisema kuwa tangu Dk. Magufuli aingie madarakani Novemba 5, 2015, hakujawahi kutokea mfumuko wa bei.

"Rais amedhibiti mfumuko wa bei, amewafutia kodi wafanyakazi ambao mishahara yao haizidi Sh. 300,000, kodi kwa watumishi wa umma ilikuwa tarakimu mbili na sasa imeshuka hadi tarakimu moja, amefanikiwa kuweka nidhamu katika matumizi pamoja na kuongeza makusanyo," alisema.

Alisema kwenye nyanja ya diplomasia, Dk. Magufuli alipoingia madarakani na kupewa uenyekiti wa Jumuiya ya Afrika Mashariki (EAC), alisimamia nidhamu na matumizi na baadaye aliteuliwa kuwa Mwenyekiti wa Jumuiya ya Maendeleo Nchi Kusini mwa Afrika (SADC) na kufanikiwa kukipigania lugha ya Kiswahili na kuimarisha Bohari Kuu ya Dawa (MSD).

"Sasa hivi dawa zote za SADC zinatoka MSD, MSD imeshonwa, imeimarishwa vizuri, nidhamu iko juu na hiyo ndiyo imesababisha kuendelea kuwa kinara katika ukanda huu. Kwa hiyo, nitoe rai ifikapo Oktoba 28, mwaka huu, Watanzania wakamchagüe Dk. Magufuli kwa maendeleo ya Tanzania," alisema Polepole.

Kuhusu hoja ya wapinzani wao kwamba wananchi wanafurika kwenye mikutano ya kampeni za CCM kwenda kuona wasanii na wengine kupelekwa kwa magari maalum, Polepole alisema:

"Mikutano yetu inakuwa na malengo mawili, kwanza tunasherehekea mafaniko ya miaka mitano pamoja na kuomba kura, hapo tunatumia wasanii kufikisha ujumbe kwa sanaa, pili tunaomba dhamana ya muhula wa pili.

"Watu wanakuja kwenye mikutano yetu kwa kujitegemea kwa usafiri na wengine wanakuja kwa miguu."

# Maalim Seif ashinda pingamizi, rasmi urais

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

MGOMBEA Urais wa Zanzibar kupitia Chama cha ACT-Wazalendo, Maalim Seif Sharif Hamad, ameshinda pingamizi lililowekwa dhidi yake kupitishwa kuwania urais katika uchaguzi wa mwaka huu.

Mwanasiasa huyo mkongwe aliwekewa pingamizi kuhusu tarehe ya kiapo chake, lakini jana Tume ya Uchaguzi Zanzibar (ZEC) ilimpitisha baada ya kushinda pingamizi hilo na kuungana na wengine 16 waliopitishwa awali.

Wakati huo, Chama cha Alliance for Democratic Change (ADC), jana kilizindua rasmi kampeni zake za kuwanadi wagombea wa Urais wa Jamuhuri ya Muungano wa Tanzania, Urais wa Zanzibar, uwakilishi, wabunge na madiwani katika Viwanja vya Mnazi Mmoja Mjini Zanzibar.

Pia, chama hicho kilizindua ilani yake ya utekelezaji ya uchaguzi kwa mwaka 2020-2025, ikiweka kipaumbele cha kujenga uchumi imara kwa manufaa ya wote.

Mgombea wa urais wa Tanzania kupitia chama hicho, Queen Cuthbert Sendiga, alisema akichaguliwa kuwa rais, atahakikisha anaongeza thamani zao la karafuu na kuwawezesha wakulima kupata fedha nyingi na kupiga hatua kiuchumi na maendeleo.

"Nikichaguliwa kuwa rais, nitahakikisha karafuu inaongezwa thamani yake ili kuwawezesha wakulima kupiga hatua kubwa ya maendeleo na kiuchumi," aliahidi.

Alisema chama chake kwa kupitia ilani yake hiyo, kimeweka vipaumbele katika mambo matatu ikiwamo kuimarisha miundombinu ya sekta ya kilimo, barabara na viwanda.

"Hayo ndiyo mambo ya msingi yaliyomo katika ilani hii... imejikita katika suala la ajira pamoja na kilimo cha viwanda kuona mazao mbalimbali yanayozalishwa yanaongezwa thamani yake," alisema.

Mwenyekiti wa ADC, Hamad Rashid Mohamed, alimkabidhi ilani ya chama hicho mgombea huyo na kumtaka kuinadi kwa wananchi


## NOTISI YA KULIPA DENI NA TANGAZO LA MNADA WA HADHARA

Kampuni ya **JAGRO ENTERPRISES LTD, WAUNGWANA AUCTION MART na KOTI BROTHERS COMPANY LIMITED** kwa niaba ya AccessBank Tanzania Limited watauza kwa njia ya mnada wa hadhara, Nyumba, Magari na Viwanja vilivyowekwa kama dhamana ya mikopo ambapo wateja husika wameshindwa kulipa mikopo yao kwa mujibu wa mikataba husika. Hivyo basi ifahamike kuwa utakapopita muda wa siku kumi na nne tangu kutoka kwa gazeti hili dhamana husika zitauzwa kwa njia ya mnada. Mnada utafanyika sehemu nyumba na viwanja husika vilipo siku na tarehe kama vilivyotajwa kwenye jedwali hapo chini.

| S/N | TAWI HUSIKA | KAMPUNI INAYO HUSIKA | JINA LA MTEJA | JINA LA MWENYE DHAMANA | AINA YA DHAMANA | MAHALI DHAMANA ILIPO | TAREHE YA MNADA |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| 1 | MBEYA | WAUNGWANA AUCTION MART | NGOBILE/A,LUSUBILO | NGOBILE/A,LUSUBILO | SHAMBA | TUKUYU | 28/09/2020 SAA 10.00 ASUBUHI |
| 2 | MBEYA | KOTI BROTHERS CO. LTD | PANGANI/O,REHEMA | PANGANI/O,REHEMA | NYUMBA | TUNDUMA | 28/09/2020 SAA 11.00 ASUBUHI |
| 3 | MBEYA | JAGRO ENTERPRISES LTD | FURAHA BAKERY | APSON/LUNDU,CORNEL | NYUMBA,MASHINE NA MAGARI | ILOMBA –NEAR VETA MBEYA | 29/09/2020 SAA 10:00 ASUBUHI |

**MASHARTI YA MNADA**

1. UKAGUZI UNARUHUSIWA MARA USOMAPO TANGAZO HILI.
2. MNUNUZI ATALAZIMIKA KULIPA MALIPO YA 25% YA FEDHA TASLIMU PAPO HAPO NA 75% BAADA YA SIKU 14 TOKA SIKU YA MNADA KUFANYIKA NA UKISHINDWA KULIPA MALIPO YALIYOBAKI MNADA UTARUDIWA NA FEDHA ULIZO LIPA HAZITARUDISHWA
3. GHARAMA ZA KUBADILISHA UMILIKI NI ZA MNUNUZI MWENYEWE, KUMBUKA VIGEZO NA MASHARTI KUZINGATIWA.

**KWA MAWASILIANO ZAIDI**
**JAGRO ENTERPRISES LTD 0754635795**
**WAUNGWANA AUCTIIN MART 0713077474**
**KOTI BROTHERS LTD 0713235517**
**WOTE MNAKARIBISHWA.**

# Majaliwa kuzindua rasmi kampeni ubunge Tanga

**Na Steven William**
MHHEZA

WAZIRI Mkuu Kassim Majaliwa anatarajiwa kuwa mgeni rasmi katika uzinduzi wa kampeni za ubunge wa Chama Cha Mapinduzi (CCM) jimbo la Tanga Mjini.

Uzinduzi huo ambao utafanyika katika uwanja wa Tangamano, ni mahususi katika harakati za kukomboa jimbo hilo kutoka mikononi mwa upinzani baada ya CCM kulipoteza miaka mitano iliyopita.

Mwenyekiti wa CCM Mkoa wa Tanga, Henry Shekifu, alisema maandalizi yote yamekamilika kampeni zitapambwa na wasanii mbalimbali wakiongozwa na Hamisi Mwinjuma, maarufu kama Mwana FA, ambaye pia ni mgombea ubunge kupitia CCM Jimbo la Muheza.

Mbali na mgeni rasmi Majaliwa, Shekifu alisema wametoa mwaliko kwa wageni kutoka sehemu mbalimbali wakiwamo wagombea ubunge majimbo mengine.

Alisema shughuli hiyo itaanza saa 1:00 asubuhi mpaka saa 12:00 jioni.

Naye mgombea ubunge jimbo la Tanga Mjini, Ummy Mwalimu, alisema tayari maandalizi ya kampeni yamekamilika na tayari vyombo vya usafiri vimewekwa stika zenye picha zake na mgombea urais, John Magufuli.

# Mgombea ubunge NCCR ajiunga CCM

**Na Thobias Mwanakatwe,**
DODOMA

MGOMBEA ubunge Jimbo la Rungwe Mkoani Mbeya kupitia NCCR-Mageuzi, Robert Mwandi, amejitoa katika kinyang'anyiro hicho na kujiunga na Chama Cha Mapinduzi (CCM).

Mwandi alijiunga CCM juzi mbele ya Makamu Mwenyekiti wa CCM (Bara), Philip Mangula, wakati akizungumza na viongozi na wanachama wa CCM kwenye mkutano uliofanyika Tukuyu mjini.

Mangula ambaye ni mlezi wa CCM Mkoa wa Mbeya, yuko katika ziara ya kutembelea majimbo yote ya mkoa huo.

Mgombea huyo akizungumza baada ya kutangaza kujitoa katika kinyang'anyiro hicho, alisema ziko sababu kuu mbili ambazo zimemsukuma kuamua kujitoa katika vyama vya upinzani.

Alizitaja sababu hizo kuwa ni vyama vya upinzani kukosa sera na mwelekeo ambao unaweza kuvifanya kuishinda CCM katika uchaguzi huu kwa sababu serikali ya CCM imefanya mambo makubwa ya maendeleo katika miaka mitano iliyopita.

Sababu ya pili, alisema ni ubinafsi ambao unaviandama vyama vingi vya upinzani, hivyo kuvifanya vishindwe kuwa na mwelekeo mzuri wa kuweza kuhimili ushindani na chama tawala.

"Kwa mfano (Bernard) Membe, mgombea urais wa ACT Wazalendo, amedumu kwenye siasa muda mrefu lakini eti sababu kura hazikutosha akiwa CCM anahamia upinzani. Huu ndio ubinafsi," alisema Mwandi.

Alisema hata mgombea urais kupitia Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA), Tundu Lissu, ni ubinafsi kuutaka urais sababu kama alishindwa kutatua kero za jimboni kwake wakati akiwa mbunge ataweza kumudu urais?

Mwenyekiti wa NCCR-Mageuzi Jimbo la Rungwe, Anyimike Mwasakilali, akizungumzia hatua ya mgombea wao kujiondoa na kujiunga na CCM, alisema jambo hilo limewasikitisha sana kwa sababu hawakutegemea kijana afanye hayo. "Huyu mgombea wetu amefanya jambo ambalo sasa watu wasiwe wanawaamini na kuwathamini vijana kupewa uongozi kwasababu wamekuwa ni vigeugeu," alisema.

Mwasakilali alisema mgombea huyo amejitoa katika kinyang'anyiro ikiwa ni siku moja tu baada ya Tume ya Taifa ya Uchaguzi (NEC) kutangaza rufani yake ya pingamizi ambapo ameshinda na kuruhusiwa kuendelea na kinyang'anyiro.



Mgombea ubunge Jimbo la Kibamba kwa tiketi ya chama cha ACT-Wazalendo, Mwesigwa Siraji, akihutubia mkutano wa kampeni za uchaguzi mkuu katika stendi ya daladala ya Mbezi Mwisho jijini Dar es Salaam, juzi. **PICHA: SABATO KASIKA**

# Sumaye aibuka na kukemea uchochezi

**Na Thobias Mwanakatwe,**
DODOMA

WAZIRI Mkuu mstaafu wa awamu ya tatu, Frederick Sumaye, ameibuka na kuitaka serikali na vyama vya siasa kuchukua hatua dhidi ya wagombea ambao wanatoa kauli zinazohatarisha kuvunjika kwa amani.

Pia amesema ushindani wa vyama na wagombea upo japo si mkali sana kulinganisha na uchaguzi uliopita.

Sumaye ambaye alikuwa akizungumza jana katika mahojiano maalum na gazeti hili, alisema amani ya Tanzania lazima idumishwe kwa kiwango chochote kile, hivyo haitakiwi mgombea au viongozi wa chama kutoa kauli ambazo zinahatarisha amani.

"Wanaotaka kuleta vurugu, kwanza vyama vyao viwashughulikie lakini kama haviwezi kuwashughulikia serikali ipo iwashughulikie," alisema Sumaye licha ya kwamba hakutaja wagombea ambao wanatoa kauli za kuhatarisha amani.

Sumaye ambaye amekuwa kimya kwa muda mrefu tangu aliporejea Chama Cha Mapinduzi (CCM) akitokea Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA), alisema wananchi kwa upande wao wawaadhibu wagombea wanaoleta vurugu kwa kutokuwapa kura.

"Hatutaki watu wanaotaka kuleta fujo kwenye nchi kwa sababu tu wanatafuta madaraka. Mgombea wa namna hiyo hafai kuwa kiongozi," alisema Sumaye.

Aliongeza kuwa amani ya Tanzania ni lazima ilindwe kwa kila mtu na si kitu cha kuchezea kwa kuwa nchi yoyote ikishapoteza amani huwa hairudi tena.

Kwa mujibu wa Sumaye, katika kipindi cha kampeni wagombea wanatakiwa kujikita zaidi katika kunadi sera za vyama vyao ili wananchi wazichuje na kuwachagua wale ambao sera zao ni nzuri.

Sumaye alisema Tanzania ndiyo nchi pekee katika Afrika ambayo wananchi wake wamekuwa wakifurahia amani kwa hiyo haitarajiwi mtu yeyote afanye mambo ambayo yanahatarisha amani ya nchi.

Alisema kiongozi yeyote anatakiwa awaonyeshe wananchi kwa kuwaletea maendeleo na si kuleta mapigano.

"Kama kuna chama ambacho kinasema sera yake ni kuleta fujo itabidi kishughulikiwe tofauti, japo najua hakuna chama ambacho kitaandikishwa kama chama cha siasa kikiwa na sera ya kuleta vurugu,"alisema.

Uchaguzi mkuu wa kuchagua madiwani, wabunge na rais umepangwa kufanyika Oktoba 28, mwaka huu, ambapo kwa hivi sasa vyama vinaendelea na kampeni.



Mgombea urais Chama Cha Wananchi (CUF), Prof. Ibrahim Lipumba, akizungumza na wananchi wa Rufiji, mkoani Pwani juzi, katika mkutano wa kampeni za uchaguzi mkuu. **PICHA: BONIFACE GIDEON**

# Saratani yaongezeka kwa waishio mijini

**Na Romana Mallya**

MKURUGENZI wa Huduma za Kinga, Taasisi ya Saratani Ocean Road (ORCI), Dk. Crispin Kahesa, amesema kuna ongezeko la saratani zinazosababishwa na mfumo wa maisha hasa kwa watu wanaoishi kwenye miji mikubwa nchini.

Dk. Kahesa aliyasema hayo jana katika mahojiano maalum na Nipashe jijini Dar es Salaam kuhusu hali ya saratani kwa sasa nchini na mikakati ya kuinusuru jamii dhidi ya baa hilo.

Alisema kwa ujumla hali ya saratani Tanzania siyo nzuri, akirejea takwimu za mwaka 2018 za Shirika la Global Fund ambalo chini ya Shirika la Afya Duniani (WHO), lilibainisha kuwa Watanzania ina wagongwa 42,060 wa saratani.

Dk. Kahesa pia alirejea takwimu za nchi za mwaka 2018/19 zinaonyesha kuna wagonjwa 12,205 waliopata huduma za matibabu ya saratani katika hospitali mbalimbali nchini na kwa ORCI pekee, wagonjwa 7,624 wanahudumiwa.

"Miaka 10 iliyopita, tukizungumzia mwaka 2010 Taasisi ya Saratani Ocean Road ilikuwa na wagonjwa wanaofika hapa 2,800. Kwa haraka, hapa pana ongezeko zaidi ya mara tatu," alisema.

Dk. Kahesa alisema aina ya saratani walizokuwa wakiziona kwa kipindi hicho ni tofauti na za sasa.

"Kipindi cha miaka 10 ya nyuma, asilimia 66 saratani zilizokuwa zinaongoza ni zile zinazoendana na maambukizi. "Vyanzo vya saratani vipo vingi na miongoni ni vya kibailojia na kusababishwa na vijidudu vinavyoleta saratani ya tumbo, shingo ya kizazi, kichwa, nyingi ziliendana na maradhi ya HIV na maambukizi mengine," alisema. Alisema kwa sasa saratani iliyo juu, bado ni ya shingo ya kizazi ingawa zile zinazosababishwa na mfumo wa maisha nazo zinapanda mfano ya matiti ambayo inashika nafasi ya pili wakati awali ilikuwa inakuwa ya tano na sita kwenye orodha ya aina za saratani zinazotesa nchini.

"Kuna tezi dume, saratani ya utumbo mkubwa nayo inapanda. Na awali tulikuwa tukizungumzia umri wa watu wanaopata saratani ni zaidi ya miaka 60 lakini kwa sasa kijana mwenye umri wa miaka 25 anayo," alisema.

Aliongeza kuwa watu wanapata visababishi vya saratani mapema, lakini ili mabadiliko yatokee na kujitokeza, kunachukua miaka 15 mpaka 20. "Inawezekana awali ili mtu akutane na visababishi, umri wake unakuwa umekwenda lakini sasa wengine wanazaliwa nayo na wengine wakifikisha umri wa miaka 25," alisema.

Mkurugenzi huyo alisema taasisi yao inaendelea kutoa elimu kwa makundi mbalimbali kwenye jamii ili wajue namna ya kujiepusha wasipate saratani.

"Tuna programu maalum shuleni ambayo imelenga kutoa elimu kwa wanafunzi ili watambue kwamba ugonjwa huu upo na visababishi vyake, lakini pia kwa wanafunzi wa vyuo wao tunawapa elimu na kuwapima kwa sababu wamefikia umri ambao kwa sasa wengi wanakutwa na tatizo hili," alisema.

Dk. Kahesa alisema mikakati mingine kama hospitali ni kuimarisha huduma za matibabu kwa kununua mashine za kisasa ambazo zitasaidia kubaini ugonjwa mapema.

# Mavunde awapa matumaini wakulima wa mboga

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

MGOMBEA Ubunge Jimbo la Dodoma Mjini kupitia Chama Cha Mapinduzi (CCM), Anthony Mavunde, ameahidi kuandaa mpango mkakati wa kuongeza tija kwenye kilimo cha mboga ili wananchi wa Ihumwa wanufaike na uwepo wa reli ya kisasa (SGR).

Akizungumza jana kwenye mkutano wa kampeni kata ya Ihumwa, Mavunde alisema eneo hilo litakuwa maarufu kwa kilimo hicho na wakulima wamekuwa wakisafirisha maeneo mbalimbali nchini ikiwamo Dar es salaam.

Mavunde Alisema mbali na kuongeza tija kwenye kilimo hicho, pia atatafuta soko la uhakika zaidi ndani na nje ya nchi ili wananchi watumie vyema fursa ya uwapo wa usafiri wa treni ya umeme. "Najua hapa kinamama ndio wazalishaji wakuu wa mboga kupeleka soko la Kariakoo la Dar es Salaam. Endapo mtanipa ridhaa tena nitahakikisha naandaa mpango maalum kwa kushirikiana na TAHA (Chama cha Wakulima wa Mboga Tanzania) ili kuongeza tija kwenye mazao yetu," alisema. Mavunde alisema hatua hiyo itabadilisha maisha ya wananchi wa kukuza kipato cha mtu mmoja mmoja. "Ndugu zangu wana Ihumwa nasimama hapa tena kuwaomba nafasi ya ubunge kupitia CCM, nikiwaomba mnipigie kura tena ili ile kazi niliyokuwa nimeianza niikamilishe hasa katika kutatua kero za msingi za kata ya Ihumwa," alisema.

Mgombea huyo pia alisema kuna tatizo la maji kwenye eneo hilo ambapo visima vikubwa vimechimbwa lakini usambazaji kwa wananchi wote bado ni tatizo.

"Wakazi wa kata ya Ihumwa naomba niwahakikishie katika bajeti ya mwaka 2020/21, Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Dodoma (Duwasa), imetenga fedha kwa ajili ya ukarabati wa miundombinu ili kuhakikisha maji yasambae katika eneo lote na wanachi waondokane na adha ya maji," alisema.

Mavunde alisema alisema akichaguliwa kuwa mbunge atahakikisha anashughulikia tatizo hilo kwa kuwa ni sehemu ya utekelezaji wa Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya mwaka 2020- 2025.

# Afungwa maisha kwa kulawiti mtoto

**Na Jumbe Ismailly,** SINGIDA

MAHAKAMA ya Hakimu Mkazi Mkoa wa Singida imemhukumu kifungo cha maisha jela mkazi wa Mtaa wa Minga, Halmashauri ya Manispaa ya Singida, Hussein Azizi (34), baada ya kukiri kosa la kumlawiti mtoto mwenye umri wa miaka minne.

Akitoa hukumu hiyo, Hakimu Mkazi Mwandamizi Robert Oguda, alisema anatoa adhabu kwa mshtakiwa ili liwe fundisho kwa watu wengine wenye tabia kama hiyo.

Awali, Mwanasheria wa Serikali, Elizabeth Barabara, alidai kwamba mshtakiwa alitenda kosa la kumlawiti mtoto mwenye umri wa miaka minne, Agosti 6, mwaka huu, katika Mtaa wa Minga.

Kwa mujibu wa mwanasheria huyo, mshtakiwa alidai kuwa watoto hao walikuwa wakimfuata hadi machungani kutokana na kuwa walimpenda sana na kwamba hakuwa amefanya tendo hilo mara moja bali alikuwa akifanya mara kwa mara.

Barabara alidai kuwa mshtakiwa huyo baada ya kusomewa shitaka lake hilo, alikiri kwamba hakuwa akifanya kitendo hicho kwa mtoto huyo peke yake bali kulikuwa na mtoto mwingine ambaye aliyefanya naye bila kugundulika.

Baada ya kusomewa mashtaka na kukiri na kabla ya kutiwa hatiani, mshtakiwa alijitetea kwa kuomba msamaha na kuahidi kwamba hatarudia tena kufanya kitendo kama hicho.

Pia katika utetezi wake, mshtakiwa alikiri kwamba kitendo alichokifanya kwa watoto hao wawili, hakikuwa kizuri, hivyo aliiomba mahakama imwonee huruma na kumpa adhabu ndogo.

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# *Barbara apimwe kwa mafanikio Simba SC*

**JUMATANO** wiki hii, Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi ya Simba Mohammed 'Mo' Dewji, alimtambulisha rasmi Barbara Gonzalez kwa wahariri wa habari za michezo nchini, kuwa Ofisa Mtendaji Mkuu wa klabu hiyo yenye makao makuu yake Msimbazi jijini Dar es Salaam.

Tangu kuteuliwa kwa Barbara katika nafasi hiyo, akirithi mikoba ya Senzo Mazingisa ambaye alijiuzulu mwezi uliopita, kumekuwa na maneno mengi mitandaoni na vyombo vya habari mbalimbali, kwa baadhi ya wadau kutia shaka uwezo wake katika nafasi hiyo.

Hofu kubwa ya baadhi ya wanachama imekuja kutokana na kile wanachodai kuwa hana uzoefu katika masuala ya soka, kama ilivyo kwa mtangulizi wake, Senzo ambaye amehudumu katika nafasi hiyo katika klabu mbalimbali lakini pia akiwa na taaluma ya ukocha. Lakini pia baadhi walifika mbali kwa kudai kwamba Barbara ambaye tangu Aprili 2016, amekuwa akihudumu kama Mkurugenzi Mtendaji wa Taasisi ya Mo Dewji Foundation, hafahamu kabisa masuala ya soka na uteuzi wake ni pendekezo la Mo, ambaye anataka kurahisisha mambo yake ndani ya klabu hiyo.

Hata, hivyo wakati akimtambulisha rasmi kwa vyombo mbalimbali vya habari jijini Dar es Salaam, Mo alisema uteuzi huo ni pendekezo la wajumbe wote wa bodi ya wakurugenzi na si yeye kama ambavyo imekuwa ikidaiwa. Kwa ujumla kukosolewa kwa Barbara kumekuwa kwingi hasa kutokana na madai ya kutokuwa na uzoefu lakini pia hilo likichangiwa na jinsi yake, wakiamini ni vigumu kwa mwanadada kubeba jukumu hilo.

Lakini, elimu ya Shahada ya Uzamili ya Usimamizi wa Maendeleo aliyoipata Chuo Kikuu cha Uchumi na Siasa jijini London, Uingereza na Shahada ya Uchumi na Siasa aliyohitimu Chuo cha Manhattanville jijini New York, Marekani inatufanya kuona ipo haja ya Barbara kupewa muda kuweza kudhihirisha uwezo wake katika nafasi hiyo badala ya kukosolewa mapema.

Lakini, imani yetu kwa Barbara inaongezeka zaidi hasa tukizingatia ukweli kwamba, alishiriki katika mchakato wa mabadiliko Simba tangu mwaka 2016, kwa kwenda Uingereza kupata uzoefu na kubadilishana maarifa ya namna klabu za huko zilivyofanikiwa kuingia katika mfumo kama huo.

Nipashe tunapinga vikali wale wanaegemea katika 'mfumo dume' wakimbeza Barbara kuwa viatu vya Senzo havitamtosha kwa sababu tu eti ni mwanamke na hajabobea katika masuala ya soka. Katika hilo tuna mifano mingi ya wanawake waliofanikiwa katika nafasi kama hiyo ya Barbara na kwenye klabu kubwa Ulaya, mmojawapo ni Marina Granovskaia, Mkurugenzi wa Klabu ya Chelsea, ambaye aliteuliwa akitoka kufanya kazi katika kampuni za mafuta za mmiliki wa klabu hiyo, Roman Abramovich.

Kama ilivyo kwa Barbara, kadhalika Marina, hakuwa na elimu yoyote ya mambo ya soka, lakini leo ndiye anayehusika katika masuala yote ya kuidhinisha wachezaji wa kusajiliwa huku akiwa amefanikisha dili kubwa ya udhamini wa Kampuni ya Nike ambayo inaiingizia klabu hiyo pauni milioni 60 kwa mwaka. Ikumbukwe pia Marina, ndiye alimuajiri Kocha Mkuu wa Chelsea, Frank Lampard, ambaye anaendelea kuisuka klabu hiyo.

Wanawake wengine ambao wanaendelea kuziongoza klabu kwa mafanikio barani Afrika ni Ofisa Mtendaji Mkuu wa AS Vita ya DR Congo, Jannifer Haid na Ainisha Muhoozi wa KCC ya Uganda, hivyo hakuna sababu ya kumbeza Barbara kwa sababu tu ya jinsi yake.


Nipashe tunasisitiza, Simba kumpa ushirikiano Barbara na yeye mwenyewe kuruhusu kuzungukwa na timu imara ya ufundi, ili kuweza kutekeleza majukumu yake hayo mapya.

Tunategemea kuona akiiwezesha Simba kupiga hatua zaidi kutoka hapo ilipofikia kwenye mchakato wao wa kuendeshwa kwa utaratibu wa mfumo wa hisa, lakini pia timu hiyo ikifanya vizuri kwenye mashindano mbalimbali inayoshiriki ya ndani na kimataifa, na hicho ndicho kiwe kipimo cha kumpima Barbara na si vinginevyo.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:

**THE GUARDIAN LIMITED**

**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782 253676
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com






Na Barnabas Maro

## Muungwana Lazima Nilonge

# *Ubaya hatima yake mbaya*

**'HATIMA'** ni mwisho wa jambo. Maana yake ubaya huwa na mwisho m-baya. Methali hii hutumiwa kutukumbusha kwamba nia mbaya au dhamira aghalabu haiwezi kufanikiwa, kwani mwisho wake huwa mbaya. Binadamu twahimizwa tuwe na nia nzuri au tusiwafanyie wenzetu mambo mabaya.

'Muungwana' ni mtu anayejistahi, mtu mwenye tabia inayokubalika katika jamii. 'Chuki' ni hisia ya kutopenda kitu au jambo. 'Chukia' (chukiana, chukiwa, chukiza) ni tabia ya mtu kutopenda mtu mwingine au kitu. 'Chukiza' ni kitendo cha kufanya jambo la kuudhi.

Kero (jambo linaloudhi) hii ndiyo inayotawala kwenye klabu za Simba na Yanga ingawa zipo kwenye nchi moja na jiji moja ambalo zamani liliitwa 'Bandari ya Salama' ambalo sasa ndilo jiji la biashara. U'wapi huo 'usalama' ilhali timu hizi zachukiana kiasi cha kufanyiana ubaya ili kuhakikisha moja inapoteza mwelekeo.

Neno 'Usiri' lina maana zaidi ya moja ila ninalolizungumzia hapa ni tabia ya kutozungumza mambo ya ndani kwa watu. Timu hizi mbili kongwe nchini na zenye wanachama na mashabiki ndani na nje ya Tanzania zashindwa kutambua umuhimu wao. Kwa hakika zingekuwa mfano mzuri kwa timu zingine nchini lakini zaoneshana ubabe, yaani ujanja na hila za kutumia nguvu; ugangwe.

Ingekuwa bora kama timu hizi zingefanya mambo yao kwa siri yaani jambo au tokeo ambalo bado halijatakiwa kudhihirishwa, kisha wanachama na mashabiki washitukie maendeleo yanayofanywa na viongozi waliowachagua. Baada ya kukamilisha shughuli za kuziendeleza katika hatua mbalimbali ndipo wafanye mikutano ya ndani na wanachama wao na kueleza mambo yaliyofanywa na kuweka wazi kiasi cha fedha zilizotumika. Kadhalika, kueleza matatizo yaliyopo klabuni na kutaka wanachama kutoa msaada wa hali na mali.

Kwa maana hiyo, wanachama wawe wanasomewa matumizi ya fedha zinazotumika kila mwaka na kuthibishwa na wakaguzi wa mahesabu. Kwa utaratibu huu watu wanaogombea nafasi za uongozi kwa lengo la kile wanachokiita 'kupiga fedha' hawatopata mpenyo wa kufanya ujanja wa kudokoa hela za klabu. Viongozi fanyeni uchunguzi tangu viongozi vimbaumbau (wenye miili myembamba, wasio na kauli ya kuaminika, vigeugeu) jinsi miili yao inavyobadilika kwa unene na vitambi!

Maana yangu ni kwamba matumizi ya fedha za klabu yakaguliwe kila mwaka na wanachama waelezwe jinsi zilivyotumika. Masuala ya fedha kulipwa wachawi yasiwapo kwani kandanda haichezwi kwa kutumia uchawi bali ni mafunzo ya walimu waliosomea jinsi ya kuwafundisha wachezaji. Kama uchawi una maana, kuna sababu zipi zinazofanya viongozi wa timu kuajiri walimu kutoka nje ya nchi na kuwalipa fedha nyingi ambazo walimu wetu wa Tanzania hawalipwi hivyo?

Mungu ndiye muumba wa vyote. "Usiwe na miungu mingine ila mimi. Usijifanyie sanamu ya kuchonga, wala mfano wa kitu chochote kilicho juu mbinguni, wala kilicho chini ya dunia; usivisujudie; wala kuvitumikia; kwa kuwa Mimi, BWANA, Mungu wako, ni Mungu, mwenye wivu; nawapatiliza wana maovu ya baba zao hata kizazi cha tatu na cha nne cha wanichukiao, nami nawarehemu maelfu elfu, wanipendao na kuzishika amri zangu."

Hao wanaoabudiwa na baadhi ya binadamu ni viumbe kama sisi. Kwa nini tunamsahau Muumba wetu na kuamini ushirikina (tabia ya kuamini uwezo wa kiumbe kingine juu yako badala ya ule wa Mwenyezi Mungu)? Kuna faida gani ya kwenda kwenye nyumba za ibada yaani makanisani na misikitini kama hatumwamini Mungu muumba wa vyote vinavyoonekana na visivyoonekana?

Kuna ushirikina mwingi uliofanywa na unaoendelea kufanywa na klabu za Simba na Yanga ili kupata ushindi na hali hiyo inaendelea hata kwa timu za mchangani! Ukioneshwa mambo yanayofanywa na klabu kubwa ili kushinda michezo yao utashangaa na kumwomba Mungu atusamehe kwa ubozi (ujuha; ujinga, upumbavu, ubaradhuli) wetu. Kadiri tunavyoyaendekeza wachawi ndivyo tunavyomsahau Muumba wetu! Tukumbuke kuwa siku za mwisho wanaoabudu wachawi na wanaoabudiwa, wote watakuwa kwenye moto wa milele!

Sasa kila timu ya Tanzania inashiriki mambo ya kishirikina. Chunguza jinsi timu zetu zinapoingia uwanjani utaelewa ninaloeleza hapa. Ni mambo ya ajabu, yanayoshangaza na kusikitisha lakini TFF imekuwa kimya bila kukemea. Si ajabu hata viongozi walipitia njia hiyo hiyo wakati walipoomba kura kwa kujua wakichaguliwa watapata nafasi ya kile kitwacho 'kupiga pesa.' Baadhi ya viongozi walitumia rushwa kuwapa wapiga kura ili wachaguliwe wakijua fika kuwa wakichaguliwa, fedha walizotoa zitarudi maradufu. Lahaula (tamko linalotumiwa na mtu anapotanabahi baada ya kusahau au kushtukia jambo)!

# Vikwazo vine vya uwekezaji vyatajwa

**Na Ibrahim Joseph,** DODOMA

SERIKALI imesema licha ya utekelezaji wa sera ya uwekezaji ya mwaka 1996 kusaidia nchi kuingia kwenye uchumi wa kati, bado kuna vikwazo vinne vinavyoikabili sekta hiyo, vikiwamo vya kikodi na visivyo vya kikodi.

Akizungumza jana wakati wa ufunguzi wa warsha ya kutathmini ya sera hiyo, Katibu Mkuu, Ofisi ya Waziri Mkuu, Dorothy Mwaluko, alisema vikwazo vingine ni uratibu wa masuala ya uwekezaji, utangazaji wa fursa za uwekezaji na uwezeshaji uwekezaji.

Mwaluko alisema serikali imeendelea kuweka mazingira wezeshi ya biashara na uwekezaji ili kuiwezesha sekta binafsi kuwa shindani.

Alisema mafanikio hayo yamedhihirisha ubora wa sera na utekelezaji wa sheria mbalimbali zinazohusika na kuhamasisha, kufanikisha na kuvutia uwekezaji nchini.

"Napenda tukumbushane kuwa hivi sasa kila nchi inafanya jitihada za kuvutia wawekezaji kwa kuweka mazingira wezeshi ya uwekezaji ili kulinda na kukuza uchumi kwa kuvutia teknolojia bora, mitaji, fedha za kigeni na kuongeza ajira katika mataifa yao, hivyo tunahitaji kuwa na sera madhubuti za kuvutia uwekezaji," alisema.

Katibu Mkuu aliwaomba wajumbe wa kikao hicho kutoa maoni ambayo nchi itapaswa kuweka mazingira wezeshi ya biashara na uwekezaji ili kuvutia wawekezaji wa ndani na nje ya nchi na kuandaa mkakati wa kitaifa wa kuvutia uwekezaji nchini.

Naye Mtafiti wa Sheria za Uwekezaji nchini, Dk. Saudin Mwakaje, alisema katika kikao hicho watatathmini hali ya uwekezaji nchini na kero zinazozikabili taasisi katika kutekeleza sera.

Alisema watapitia sera mbalimbali na kuona kama zinaendana na hali ya sasa na kama kutakuwa na uhitaji watatoa mapendekezo ya kuzibadili ili ziendane na wakati wa sasa.

"Tuna sera ambayo ilipitishwa mwaka 1996 ndiyo tutaijadili utekelezaji wake. Tunajua kuna mabadiliko mengi ya sheria ambayo yanaathiri utekelezaji wa sera za uwekezaji, hivyo tutajadili mafanikio na changamoto kuboresha sera hizo," alisema.

# TCRA yafunga Wasafi FM kwa siku saba

**Na Beatrice Shayo**

MAMLAKA ya Mawasiliano (TCRA), imesitisha utoaji huduma za utangazaji za Wasafi FM kwa muda wa siku saba, baada ya kubainika kutumia lugha ya matusi na isiyo na staha kwa jamii katika kipindi chake cha 'The Switch' na Mashamsham.

Vilevile, TCRA imekitaka kituo hicho cha redio kusitisha matangazo yake yote ya jana kuanzia agizo lilipotoka jana mchana na kutumia muda huo kuomba radhi kwa umma wa Tanzania kwa kukiuka kanuni za utangazaji.

Akizungumza na waandishi wa habari jana jijini Dar es Salaam, Mkurugenzi Mkuu wa TCRA, James Kilaba, alisema endapo Wasafi FM itashindwa ama kukaidi uamuzi huo, hatua zaidi za kisheria na kiudhibiti zitachukuliwa.

Kilaba alisema watangazaji hao wametumia lugha yenye matusi ambayo hata yeye hawezi kuyanukuu na kufanya hivyo ni kinyume cha kanuni namba 11(1)(c) na (d) za Kanuni za Mawasiliano ya Kieletroniki na Posta za Mwaka 2018.

Alisema maudhui ya utangazaji wa redio na televisheni zinamtaka mtoa huduma wa maudhui kuhakikisha kuwa anatangaza maudhui yenye lugha za staha.

"Mtoa huduma ya maudhui anapaswa kufuata sheria, kanuni na masharti ya leseni sambamba na maelezo yanayotolewa na mamlaka ya mawasiliano Tanzania katika utangazaji na maudhui yake," alisema.

Mkurugenzi huyo alibainisha kuwa kutokana na ukiukwaji wa kanuni,wameamua kuwachukulia hatua Wasafi FM na kuwataka watangazaji kuzingatia maadili.

"Ikumbukwe kwamba uamuzi wa namna hii siyo kiwango cha makosa mtakayoendelea kuyatenda. Niendelee kutoa rai kwa vyombo vya utangazaji vyote na watangazaji wake kuzingatia kanuni zote za utangazaji kwa lengo la kulinda maslahi mapana ya nchi yetu kimaadili," alisema.



Mwenyekiti wa Asasi ya Agenda ya Vijana Tanzania, Rogers Fungo, akizungumza kwenye mkutano wa uchaguzi wa viongozi wa Jukwaa la wanaharakati wa haki za vijana wanawake, uliofanyika makao makuu ya Mtandao wa Jinsia Tanzania (TGNP), Mabibo, jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: SABATO KASIKA**

# NICOL yatoa gawio kwa wanahisa

**Na Mwandishi Wetu**

KAMPUNI ya National Investments Plc (NICOL), imetoa gawio kwa wanahisa wake la miaka mitatu iliyopita hali inayodhihirisha kuendelea kuimarika kwa kampuni hiyo.

Kwa mujibu wa taarifa iliyotolewa na kampuni hiyo jana, gawio hilo ni kwa mwaka 2016, 2017 na 2018 fedha ambazo zimelipwa kupitia akaunti ya benki ya kila mwanahisa.

"Tunapenda kuwatangazia wanahisa wote kwamba kama ilivyoidhinishwa kwenye mikutano mikuu iliyopita ya wanahisa tumefanya malipo hayo kwa kila mwanachama," ilisema.

Taarifa hiyo iliwataka wanahisa ambao hawajapokea gawio kuwasilisha nyaraka za umiliki wa hisa pamoja na taarifa za benki ili kulipwa magawio yao.

"Wanachama wetu ambao hawajapata gawio wawasilishe nyaraka zao za umiliki wa hisa na taarifa za akaunti zao kabla ya Septemba 30, mwaka huu, na fomu ya gawio inapatikana kwenye tovuti yetu," ilisema taarifa hiyo.

Taarifa hiyo pia ilisema kampuni hiyo ilianzishwa mwaka 2001 na wanahisa wachache ambao walitoa michango yao lengo ikiwa ni kuwawezesha wananchi kumiliki uchumi.

Ilisema tangu kuanzishwa kwake, kampuni hiyo haikuwahi kutoa gawio hadi wananchi walipolalamika na kuchagua uongozi mpya mwaka 2012 ambapo Dk. Gideon Kaunda alichaguliwa kuwa Mwenyekiti wa Bodi.

Ilisema pamoja na changamoto mbalimbali uongozi huo mpya ulianza kutoa gawio la kwanza mwaka 2016 la Sh 25, mwaka 2017 gawio la Sh 26 na mwaka 2018 gawio la Sh. sita ambapo ilifanikiwa kulipa madai na malimbikizo na kodi serikali Sh. bilioni 1.5.

Ilisema katika kuendelea kuhakikisha inalipa gawio zuri kwa wanahisa wake, NICOL imejiwekea mikakati mipya ya kuikuza kampuni hiyo na kuwa miongoni mwa kampuni kubwa hapa nchini zinazolipa kodi na kutoa gawio zuri kwa wanahisa wake.

"Uongozi mpya wa bodi chini ya uongozi wa Dk. Kaunda umefanya mageuzi makubwa na unaendelea kujidhatiti na kuweka mikakati kuhakikisha kampuni inaendelea kuwa imara ili kuwanufaisha wanahisa wake," ilisema.

# Selimundu bado tishio SADC

**Na Christina Mwakangale**

NCHI zilizopo Kusini mwa Jangwa la Sahara, zina idadi kubwa ya wagonjwa wa selimundu hususan watoto walio chini ya miaka mitano.

Kati ya watoto 300,000 hadi 500,000 wenye ugonjwa huo huzaliwa kila mwaka duniani, huku zaidi ya asilimia 70 wakizaliwa katika nchi za Kusini mwa Sahara.

Mkurugenzi Mtendaji wa Asasi zinazojishughulisha na Ugonjwa wa Selimundu Tanzania (TANSCDA), Dk. Deogratius Soka, aliyasema hayo jana wakati akizungumza na Nipashe, kuhusu mwezi Septemba ambao ni maalum kwa uelimishaji ugonjwa huo duniani.

Alisema ugonjwa wa selimundu, kwa hapa nchini unachangia vifo vya watoto wenye umri wa miaka mitano kwa asilimia 6.7.

"Ugonjwa huu wa kurithi, hurithiwa katika njia sawa sawa na mtu anavyorithi rangi yake ya mwili au macho, urefu, mtu huzaliwa na ugonjwa huu. Selimundu huathiri mamilioni ya watu duniani kote na hasa wale wanatoka Jangwa la Sahara," alisema Dk. Soka.

Alisema Tanzania ni moja ya nchi zenye wagonjwa wengi duniani, inakadiriwa kati ya watoto 8,000 hadi 11,000 wanazaliwa na ugonjwa huo kila mwaka.

"Inakadiriwa kuwa asilimia 15 hadi 20 ya watu wote nchini wana vinasaba vya ugonjwa wa selimundu. Watoto wanane kati ya watoto 1,000 wanaozaliwa, huzaliwa na ugonjwa huu.

Tanzania inashika nafasi ya nne duniani kwa wingi wa wagonjwa wa selimundu, nyuma ya Nigeria, India na Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo (DRC)," alisema Dk. Soka.

Dk. Soka alisema kuwa wagonjwa wenye ugonjwa huo, huwa na upungufu wa damu, kupata maambukizi ya vimelea vya magonjwa ikiwamo homa ya uti wa mgongo na watoto kupata nimonia huku watu wazima wakikumbwa na kiharusi.

"Chembe nyekundu za selimundu hushindwa kupita kwa urahisi katika mishipa midogo ya damu na hivyo kukwama na kuziba mzunguko wa damu. Hali hii husababisha maumivu yenye ukali tofauti, pia kukwama na kuziba mzunguko wa damu kwenda kwenye kichwa husababisha kiharusi," alisema Dk. Soka.

Kadhalika Dk. Soka aliiasa jamii kuacha kunyanyapaa wagonjwa wa selimundu kwa kuwa na dhana kuwa, wenye ugonjwa huo hawawezi kujihusisha na mahusiano, kuolewa na hata kuzaa watoto.




Gari la maji likisambaza huduma hiyo kwa wakazi wa eneo la Goba Tegeta A, jijini Dar es Salaam mapema wiki hii. Ndoo moja inauzwa 300/-.
**PICHA: MIRAJI MSALA**

# Wakazi DDC walalamikia harufu majitaka

**Na Frank Maxmillian,** TUDARCo

WAKAZI wa mtaa wa DDC Manispaa ya Kinondoni, jijini Dar Es Salaam, wamelalamikia kero ya maji machafu na harufu kali kutokana na mitaro inayopitisha maji hayo kujaa kiasi cha kusambaa kwenye makazi ya watu.

Baadhi ya wakazi wa eneo hilo wakizungumza na Nipashe jana kwa nyakati tofauti, walisema maji hayo yanayotoa harufu kali yamejaa kwenye barabara inayokatisha mtaani hapo na kusababisha hofu ya kukumbwa na magonjwa ya mlipuko.

Walisema hali ambayo iliyoanza mwanzoni mwa mwezi huu, imekuwa kero kwao kiasi cha kuhatarisha afya zao, hasa watoto.

"Maji hayo yamekuwa yakitiririka mfululizo, hivyo kusababisha eneo kuwa chafu na hatarishi hasa kwa watoto waishio," alisema Emmanuel Sanga.

"Tumezungumza sana kuhusu hali iliyotokea hapa mtaani, lakini DAWASA (Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Dar es Salaam) hawajatufikia kutupatia msaada. Inanipa shida zaidi kwa sababu hili ni eneo langu la biashara," alisema Rosemary Chacha.

Wakizungumzia kero hiyo, Mwenyekiti wa Mtaa huo, Selemani Masale na Bibi Afya wa Mtaa, Nancy Zakayo, walisema maji hayo ni changamoto kubwa kwa wakazi wa DDC na kuiomba DAWASA kushughulikia suala hilo haraka iwezekanavyo.

"Majitaka hayo ni hatari kwa afya hasa za watoto wachezao eneo hilo, hivyo basi linapaswa kushughulikiwa mapema," alisisitiza Zakayo.

Mwandishi wa habari hii alishuhudia majitaka yakiwa yamesambaa mtaani huku kukiwa na harufu kali na huku wananchi wakiendelea na shughuli zao wakipata shida kupita barabarani.

Akizungumzia suala hilo, Msemaji wa DAWASA, Evalyster Lyaro, alisema "tatizo tumelipokea na tupo mbioni kulifanyia kazi katika kulinda usafi wa mazingira."

## Huduma majisafi kuboreshwa zaidi

**Na Happy Severine,** BARIADI

UPATIKANAJI wa huduma ya majisafi na salama Mkoani Simiyu unatarajiwa kuongezeka kutoka asilimia 51 ya mwaka 2019 hadi 57.4 ifikapo mwezi ujao.

Hatua hiyo inatokana na mafanikio ya mradi wa lipa kulingana na matokeo (PF4R ) hali itakayosaidia wananchi kuepukana na adha ya upatikanaji wa huduma hiyo kwa uhakika na urahisi.

Mbali na ongezeko hilo, pia kutakuwapo na ongezeko la ajira kwa wananchi ambao watajipatia kazi kupitia mradi wa usambazaji wa mabomba katika miradi 23 ya mradi huo.

Hayo yalisemwa jana na Meneja wa Wakala wa Maji na Usafi wa Mazingira Vijijini (RUWASA), Mhandisi Mariam Majala, wakati wa makabidhiano ya mabomba yatakayotumika kutekeleza miradi ya maji mkoani hapa yaliyofanyika katika ofisi za RUWASA mjini hapa.

Mhandisi Majala alisema mpaka sasa wamepokea asilimia 70 ya mabomba ya maji yenye thamani ya Sh. Milioni 823 ambayo yatatumika kutekeleza miradi 23 kwa mkoa mzima huku wakisubiri wakati wowote kuwasili kwa asilimia 30 ya mabomba yaliyobaki.

Aliongeza kuwa hali ya upatikanaji wa huduma ya maji kwa sasa si mbaya na wanawahakikishia wananchi ongezeko kubwa la huduma hiyo.

Awali, akikagua mabomba hayo, Katibu Tawala wa Mkoa wa Simiyu, Mariam Mmbaga, aliwataka wananchi kushiriki kwenye mradi huo kwa kutunza miundombinu ili lengo la ongezeko hilo walilokusudia lifikiwe.

Mjumbe wa Bodi ya Ununuzi, Ekwabi Mujungu, aliomba kazi ifanyike kama ilivyopagwa ili thamani ya fedha ionekane.





# NEC yaonya asasi elimu ya mpigakura

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

TUME ya Taifa ya Uchaguzi (NEC) imezionya asasi za kiraia, ambazo hazijapatiwa kibali cha kutoa elimu kwa mpigakura kutojihusisha na shughuli zozote za uchaguzi mkuu kwa kuwa kufanya hivyo ni kosa la jinai.

Ofisa wa Sheria wa NEC, Richard Lugomela, alitoa onyo hilo jana kwenye uzinduzi wa elimu ya mpigakura uliofanywa na Shirika la Elimu ya Amani Tanzania.

Lugomela alisema tume hiyo haitasita kuchukua hatua za kisheria kwa asasi na mashirika yote yatakayojihusisha na uvunjifu huo wa sheria, kanuni na taratibu za uchaguzi.

"Kwa asasi ambayo bado haina kibali kutoka NEC, haitakiwi kabisa kufanya shughuli yoyote ya kutoa elimu ya mpigakura katika uchaguzi mkuu mwaka huu vinginevyo itakuwa imejiingiza katika jinai na sheria zitachukuliwa dhidi yake," alisema Lugomela.

Kadhalika, alisema kwa asasi yoyote ambayo imepatiwa kibali cha kutoa elimu ya mpigakura katika uchaguzi mkuu, haipaswi kuingia ubia na asasi ambayo haina kibali.

"Asasi ambayo itakiuka sheria, kanuni na taratibu za Tume ya Taifa ya Uchaguzi, hatua kali zitachukuliwa ikiwa ni pamoja na kufutiwa usajili wake," alisema Lugomela.

Pia alisema asasi za kiraia zinatakiwa kutoa elimu ya mpigakura kwa mujibu wa vibali ilivyoomba na si vinginevyo.

Aidha, alisema NEC inatarajia kuona asasi zote zilizopatiwa vibali hazitajihusisha na kampeni za kisiasa na kuacha majukumu yao kwa mujibu wa sheria.

"Ni matumaini yangu kuwa asasi hazitajingiingiza kuwa upande mmoja wa chama katika uchaguzi, kwani kujiingiza katika chama kimoja itakuwa imewanyima haki wananchi wengine," alifafanua.

Lugomela alisema wanatarajia uchaguzi mkuu mwaka huu kuwa huru na wa haki na hawategemei asasi za kiraia kuwa chanzo cha uvunjifu wa amani.

Naye Ofisa Uhamasishaji wa Shirika hilo, Hamisi Kiyogoma, alisema lengo la kutoa elimu hiyo ni kuhakikisha kuwa uchaguzi mkuu 2020 unafanyika kwa amani bila kikwazo chochote.

"Elimu hii tunaitoa nchi nzima, katika mikoa yote kwa kushirikiana na NEC ili wananchi watambue umuhimu wa kushiriki kupiga kura na kutambua thamani ya kura yao," alisema Kiyogoma.



Wakulima wakitumia trekta kupura uwele, badala ya kupigapiga na fimbo, katika eneo la Busi, Halmashauri ya Kondoa, mkoani Dodoma juzi. **PICHA IBRAHIM JOSEPH**

## Askofu atahadharisha wanawake uchaguzi

**Na Peter Mkwavila,** DODOMA

ASKOFU wa Kanisa la International Evangelism Tanzania (IEC), Jimbo la Morogoro, Lucy Londo, amewataka wanawake wanaliojiandikisha kupiga kura, kuhakikisha wanawachagua viongozi bora kenye uchaguzi mkuu wa mwaka huu.

Askofu Londo aliyasema hayo jana alipokuwa akizungumza na waandishi wa habari jijini hapa.

Londo alisema wanawake hao wanapaswa kujitokeza kwa wingi siku ya kupiga kura ili kuwachagua viongozi watakaofaa kwa ajili ya maendeleo ya taifa na si vinginevyo.

"Pia wanawake tuendelee na maombi kila siku bila kuchoka kwa ajili ya kuombea uchaguzi mkuu utakaofanyika mwaka huu ili taifa lipate viongozi watakaotokana na chaguo la Mungu," alisema.

Naye Mwenyekiti wa Idara ya Wanawake Watumishi wa Kanisa hilo, Mchungaji Martha Mbisse, aliwataka wagombea kunadi sera zao kistaarabu kwenye majukwaa ya kampeni bila kutumia lugha za uchochezi na matusi.

Mbisse alisema wanawake wa kanisa hilo watachagua viongozi wenye sera zinazokubalika zinazowaletea maendeleo na si wanaotumia matusi na watoa rushwa.

"Tunataka wagombea wa vyama vya siasa katika kipindi hiki cha kuelekea uchaguzi wa viongozi vwa vyama vya siasa kufanya kampeni za kistaarabu na siyo zenye lugha chafu," alisema.

# Serikali yazindua muundo ustawi wa jamii

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

SERIKALI imezindua muundo wa utumishi wa kada ya ustawi wa jamii na miongozo saba ya huduma za ustawi wa jamii ikiwamo uanzishaji na uendeshaji wa makazi ya wazee na wasiojiweza.

Kutokana na hilo, imezionya taasisi binafsi kutotumia fursa hiyo kibiashara bali zinapaswa kutoa kama huduma kwa wazee.

Akizindua miongozo hiyo jana, Katibu Mkuu wa Wizara ya Afya, Idara Kuu ya Maendeleo ya Jamii, Dk. John Jingu, alisema pamoja na serikali kuwa na nyumba za wazee 17, imekuwa ikipokea maombi kutoka taasisi hasa mashirika ya kidini kutaka kuanzisha makazi hayo.

"Hadi sasa kuna makazi 18 binafsi ya wasiojiweza. Sasa tumetoa mwongozo ambao utaweka utaratibu mzuri na viwango ili isije mtu akatengeneza kibiashara. Hii ni huduma siyo biashara ni kuwasaidia wazee," alisema.

Dk. Jingu alifafanua kuwa miongozo hiyo imetengenezwa baada ya kufanya utafiti na kutumia mbinu mbalimbali za kisayansi ili kupata vitu vitakavyosaidia kuwa na miongozo bora.

"Huduma bora za ustawi wa jamii ndio msingi wa taifa. Familia zikiimarika na taifa linakuwa imara, zikiyumba na taifa linayumba. Tuna jukumu kubwa la kuhakikisha huduma zinaimarika na kwa kufanya hivyo ndiyo tumekuja na miongozo mbalimbali," alisema.

Alisema kati ya miongozo hiyo saba kuna wa uanzishaji wa nyumba salama kwa ajili ya wahanga wa ukatili na usafirishaji wa binadamu.

"Kwa mfano mtoto amefanyiwa ukatili mkubwa na mzazi kumwacha pale si salama na ni kumhatarisha mtoto. Sasa tunaanzisha nyumba ambazo zitatoa hifadhi ya muda kwa mtu wa aina hiyo wakati suala lake linashughulikiwa na watapata huduma zinazostahili ikiwemo za unasihi,"alisema.

Pia alisema kuna mwongozo unatoa fursa ya kuwa na wawakilishi wa watoto mahakamani ambao ni wasaidizi wa kisheria huku uwepo wao ukinufaisha watoto 700 na huduma za kisheria.

"Kuna mwongozo wa programu za kijamii za marekebisho ya tabia kwa watoto waliokinzana na sheria na wale walio katika hatari ya kukinzana na sheria ambapo huu unaweka utaratibu wa uanzishaji, uendeshaji na usimamizi wa vituo baada ya kuwachepusha watoto kutoka mfumo wa jinai," alisema.

Mingine ni wa kuwaunganisha watoto na familia zao, utambuzi wa huduma kwa watoto walio katika mazingira hatarishi na mwongozo wa majukumu ya maofisa ustawi wa jamii katika mamlaka za serikali za mitaa.


Kuhusu muundo wa utumishi wa kada ya ustawi wa jamii, alisema lengo lake ni kubainisha kwa kina majukumu hasa ya maofisa ustawi wa jamii ili kuondoa mkanganyiko uliokuwapo wa kufanya kazi zilizopaswa kufanywa na ofisa maendeleo ya jamii au mtu mwingine.

"Pia muundo utasaidia vyuo vyetu vinavyotoa taaluma ambazo ni muhimu katika fani za ustawi wa jamii waimarishe mitaala yao. Hatuwezi kujua ni watu wa aina gani tunahitaji katika kada ya ustawi wa jamii na hapa tumeboresha na kuongeza idadi ya fani ambazo zinastahili na hatua hiyo itaongeza ajira," alisema.

Naye Mwakilishi Mkazi wa Shirika la Kimataifa la Uhamiaji (IOM), Dk. Qasim Sufi, alisema duniani kuna waathirika takribani milioni 20.9 wanaolazimishwa kufanya kazi na usafirishaji haramu wa binadamu jambo ambalo linapaswa kukomeshwa.

"Wahanga (waathirika) wanasafirishwa kutoka vijijini hadi mijini kwa ajili ya kazi na kunyanyaswa kijinsi. Waathirika wa biashara haramu na walionusurika na ukatili wa kijinsia na watoto wako kwenye hatari na wanahitaji ulinzi kutokana na vitisho wanavyopata, hivyo kwa kushirikiana na wizara imetengenezwa miongozo hii ili kutokomeza ukatili huo,"alisema.

Mkurugenzi Msaidizi wa Idara ya Afya, Ustawi wa Jamii na Lishe kutoka Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), Rashid Maftaha, alisema ofisi hiyo imejipanga kuhakikisha miongozo hiyo inatekelezwa ipasavyo.





# CCM kuwasha moto wa kampeni Zanzibar

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

CHAMA Cha Mapinduzi (CCM) leo kinatarajiwa kuzindua kampeni zake huku mgombea wake wa urais Zanzibar, Dk. Hussein Mwinyi, akitazamiwa kutangaza Ilani ya chama hicho kwa wananchi.

Naibu Katibu Mkuu wa CCM Zanzibar, Dk. Abdalla Juma Sadala, aliwaambia waandishi wa habari jana kuwa uzinduzi huo unatarajiwa kufanyika katika Viwanja vya Demokrasia, Kibanda Maiti.

Alisema kazi ya uzinduzi huo unatarajiwa kuongozwa na Makamu Mwenyekiti wa CCm Zanzibar, Dk. Ali Mohamed Shein, ambaye atamtambulisha mgombea wa CCM.

"Napenda kuwajulisha wananchi kwamba CCM Zanzibar inatarajia kufanya mkutano mkubwa wa uzinduzi wa kampeni zake. Mgombea wa urais wa Zanzibar kwa tiketi ya CCM, Dk. Hussein Ali Mwinyi, atatambulishwa kwa wapigakura," alisema.

Aliwataka wananchi, wanachama na wafuasi wa chama hicho kujitokeza kwa wingi katika uzinduzi huo.

"Mkutano huu licha ya kumtambulisha mgombea wetu wa urais wa Zanzibar, Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya mwaka 2020-2025 itazinduliwa kwa wapigakura ili waweze kuifahamu na kuifanyia kazi. Ilani hii imejikita katika mambo muhimu ya maendeleo, uchumi na ustawi wa jamii," alisema.

Pia alisema katika mkutano huo, vikundi mbalimbali vya sanaa, vinavyowajumuisha vijana wa kizazi kipya, vitatoa burudani kwa wananchi na wanachama watakaohudhuria.

Baada ya uzinduzi huo, alisema mikutano mingine ya kampeni inatarajiwa kufanyika Unguja na Pemba huku wagombea wa chama wakiwamo wabunge, wawakilishi na madiwani watafanya mikutano katika majimbo ya uchaguzi.

Kiongozi huyo alisema CCM itafanya kampeni za kistaarabu, hivyo aliwataka viongozi wa vyama vingine vya siasa kufanya kampeni ambazo hazitachochea fujo wala vurugu na badala yake kufanya kampeni zitakazohamasisha amani ya nchi.



Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Dk. Ali Mohamed Shein (kulia) na Mgombea Urais wa Zanzibar kwa tiketi ya Chama Cha Mapinduzi (CCM), Dk. Hussein Mwinyi (wa pili kulia), Mke wa Rais Mama Mwanamwema Shein (wa tatu kulia) na Mke wa Mgombea Urais Mama Maryam Mwinyi (wa pili kushto), wakisoma ratiba ya hafla ya taarab maalum ilioandaliwa na chama hicho, katika ukumbi wa Sheikh Idrisa Abdulwakil Kikwajuni, mjini Zanzibar juzi usiku. **PICHA: IKULU**

# Waziri ajivunia huduma ya afya kidigitali

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

WAZIRI wa Afya, Hamad Rashid Muhammed, amesema hatua ya kuanzisha huduma za afya kwa njia ya digitali ni moja ya maendeleo makubwa ndani ya Zanzibar.

Alisema mfumo huo ni umuhimu ambao utazitambua taarifa na takwimu mbalimbali za wagonjwa wanaougua maradhi mbalimbali ambao hufika vituo vya afya kupatiwa matibabu.

Hamad alisema hayo jana mjini hapa wakati akizindua mkakati wa digitali wa afya huku akibainisha kuwa mfumo huo utakuwa na umuhimu wake kwa vile sasa dunia inaelekea katika mambo ya teknolojia .

Alisema mabadiliko ya maendeleo hayo hayakutokea kwa siku moja bali ni ya miaka mingi na hata Shirika la Afya Duniani (WHO) linalitambua hilo.

Hamad alisema uwapo wa huduma za afya za kidigitali utawezesha kuongeza nguvu za utoaji wa huduma kwa jamii.

Waziri huyo alisema katika kuendelea na mfumo huo wananchi wa Zanzibar sasa hawapati shida tena iwapo mfumo huo utakuwa unaeenda kama ulivyotarajiwa.

Alisema katika kasi ya kuendana na mfumo huo, lazima mitambo ya kisasa ipate nafasi katika ukuaji na uendeshaji wa mfumo huo.

Pia alisema mfumo huo hautakuwa na maana yoyote iwapo serikali haijafanya jitihada za makusudi kuwasomesha wanafunzi wa shule na vyuo vya afya juu ya mfumo huo.

Naye Mkurugenzi na Uendeshaji wa Utumishi, Ramadhan Khamis Juma, alisema iwapo mfumo huo utafanya kazi kama ulivyotarajiwa, utaokoa muda katika kutoa matabibu kwa wagonjwa na kuokoa gharama.

Mwakilishi wa WHO, Dk. Andemi Chael Ghairinay, alisema katika kufikia malengo ya mfumo huo, lazima kuwashirikisha wananchi na kwa Zanzibar itakuwa moja ya mipango ya kuwasogezea wananchi huduma bora za matibabu.

## Sababu maradhi yasiyoambukiza zawekwa wazi

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

MOJA ya sababu za kuongezeka kwa maradhi yasiyoambukiza Zanzibar ni jamii kuacha kutumia vyakula vya asili na kutumia zaidi vile vya makopo ambavyo vina kemikali.

Mkuu wa Kitengo cha Maradhi ya Kisukari, Dk. Faiza Kassim Suleiman, alisema hayo jana wakati akizungumza na waandishi wa habari katika ukumbi wa Malaria, Mwanakwerekwe wakati wa mkutano wa wadau wa maradhi hayo.

Alisema kubadilika kwa mfumo wa maisha na wananchi kula chakula bila mpangalio kumesababisha kiwango kikubwa cha maradhi yasiyoambukiza ambayo yamekuwa yakipoteza maisha ya watu wengi. Dk. Faiza aliitaka jamii kupunguza matumizi ya vyakula vya makopo ambavyo haviimarishi afya zao na kuwashauri wananchi kutumia zaidi matunda na mboga huku wakitilia mkazo kufanya mazoezi kuimarisha afya zao.

Mratibu wa Maradhi Yasiyoambukiza, Omar Abdalla Ali, alisema hatua zinazochukuliwa ni pamoja na kutoa elimu na ushauri kwa jamii.

Alisema kwa mujibu wa utafiti uliofanyika Zanzibar mwaka 2011, kati ya watu 100, 33 wamegunduliwa na maradhi yasiyoambukiza wenye umri wa miaka 25 hadi 69.

Omar aliyataja maradhi yasioambukiza ambayo yanaongoza zaidi ni kisukari, shinikizo la damu, saratani ya shingo ya kizazi, saratani ya tenzi dume, saratani ya matiti, ajali za barabarani na matatizo ya meno. Alisema kinamama 12,212 waliofika kuchunguzwa saratani ya shingo ya kizazi katika Hospitali ya Rufani ya Mnazi Mmoja, 371 sawa na asilimia tatu waligundulika na maradhi hayo na 34 walipelekwa Ocean Road kwa matibabu zaidi.

Naye Dk, Suleiman Selele, Mratibu wa Tamasha la Vyakula vya Asili, alisema ushirikishwaji wa jamii katika masuala ya kiafya utasaidia utumiaji wa vyakula vilivyo sahihi ambavyo havina vichocheo vya maradhi yasioambukiza.



KUMBE BURNA BOY, STEFFLON NI MKE NA MUME?

Ukurasa.14

Nipashe MWANGA WA JAMII
BT





KILLY&CHEED

# Wameshindwa pera kwa Ali Kiba, wataweza tufaa la Konde Boy?

WALIPOONDOKA katika lebo ya Kings Music, Wanamuziki Killy na Cheed, walikuwa na mengi ya kujitetea ikiwamo kile walichosisitiza kwamba wao wanafuata ushauri wa wazazi wao.

Wengi walishangaa sababu hiyo, wengine walihoji kwa nini wasanii wote waondoke na sababu iwe moja? Lakini kwa wale waelewa walijua safari hiyo kuna nahodha anawaongoza.

Pamoja na kuacha ghafla katika lebo hiyo iliyowatangaza, Ali Kiba ambaye ndiye kiongozi, hakuwa na maneno mengi badala yake aliwatakia safari njema na kuwashukuru kwa kumtambua kama ndiye aliyewaibua.

Juma hili, wasanii hao waliibuka tena, safari hii walitangaza kujiunga na lebo ya Konde Gang, ambayo bosi wake ni mwanamuziki Harmonize.

Katika ujumbe wa wasanii hao wakati wakijiunga na lebo hiyo, walimshukuru sana Ali Kiba kwa kuwatoa kimuziki, pia wakamsifu Harmonize, kwa kuwakubalia wajiunge katika kundi hilo kubwa.

Harmonize, aliwakaribisha kwa ujumbe wenye nasaha na angalizo makini kwa vijana hao.

" Karibuni Killy na Cheed, silaha yetu ni upendo pamoja na kazi, maana hizo ndiyo haja za wananchi wanaoifanya leo hii Konde Gang Music kuwa ulimwenguni, Konde Gan ni lebo kubwa kwa hiyo acha tufanye".

Killy na Cheed wanakumbushwa kwamba pamoja na furaha ya kujiunga na Konde Gang, lakini wakumbuke kwamba ni lazima wachape kazi na kuacha utoto unaofanywa na watoto pacha.

Huko sasa hakutakuwa na mfumo wao wa 'wawili' kila mmoja atambue umuhimu wake na watakula kutokana na kazi wanazofanya na si vinginevyo.

Wakitaka kufanikiwa ni lazima waache 'upacha' wao kwani wakiendelea na mtindo huo watajikuta wakikumbuka 'pera' walioacha kula kule kwa Ali Kiba na kukimbilia 'Tufaa' la Harmonize ambalo watashindwa kutafuna.

BASI SAWA

## Joshen awachezesha ‘Jini Baba’



MSANII chipukizi wa muziki wa Bongo Fleva,Joshen Adam, maarufu kama ‘Giny’amekamilisha singo yake mpya inayoitwa ‘Jini Baba’.

Akizungumza na BT, msanii huyo amesema wimbo huo umetayarishwa katika studio ya Asset Music chini ya prodyuza ‘Kazu Beats’ ya jijini Dar es Salaam.

Amesema wimbo huo ambao upo katika mfumo wa ‘Audio’utaanza kusikika hivi karibuni baaada ya utaratibu wa kuutambulisha rasmi kufanyika.

“Nipo kwenye gemu kwa muda mrefu lakini kupitia wimbo huu, mashabiki wa muziki watarajie kupata radha mpya yenye kuleta mabadiliko katika muziki,” amesema Gyni.

## Supa Marioo kwa nini ulimpiga tunda lako?

MSANII wa filamu za Bongo Muvi, Niva Supa Marioo, amesema kitendo cha kumfumania mpenzi wake kilimfanya kulala mahabusu baada ya kutembeza kipigo.

Niva Marioo, amesema alipelekwa mahabusu mara mbili mara ya kwanza ni baada ya kumfumania mpenzi wake, mara ya pili alikamatwa baada ya kwenda kufanya shoo na marehemu Udeude.



“Kwenye maisha yangu sijawahi kwenda jela, ila polisi na mahabusu niliwahi kuingia mara mbili, kosa la mara ya kwanza ilikuwa kumpiga Ex wangu ambaye nilimfumania, kama unavyojua unapomfumania mtu unakua kama kichaa, tena nilimfuma akiwa anapigwa kisi na mwanaume mwingine kwenye gari, nilikuwa nimemfuata tukafurahi kula bata ila nikajikuta nimelala kituoni”

Niva Marioo amesema baada ya tukio hilo kutokea alikaa chini na kujutia kwa sababu ndiyo ilimfanya kwenda polisi kwa mara ya kwanza.



## Haya Uchebe ndo kasema, Shilole kaa eda

ALIYEKUWA mume wa mwanamuziki na mjasiriamali, Shilole, ameibuka na kusema msanii huyo anatakiwa kufuata taratibu za kidini kwa kukaa eda baada ya kupewa talaka.

Akizungumza na East Africa radio, Uchebe amesema amempa talaka Shilole kwa awamu kama imani ya Kiislam inavyotaka, hivyo ni lazima naye kufuata kwa kukaa eda ili yeye ampatie huduma zote muhimu.

“Matatizo yanaponikuta huwa namuomba sana Mungu nisifanye jambo la ajabu, maana wanawake wana vitu viwili, kwanza anapomkosea mumewe hakubali anataka kushindana naye na kwenye ndoa ndiyo inawabeba sana” amesema Uchebe

Halafu akamalizia “Sipo karibu na mwenzangu na nimetoa talaka ambazo zina awamu, pia anatakiwa akae eda kupata huduma, ukitaka kuoa kuna misingi mingi unatakiwa kuifuata”.



## Mmh! Amber Lulu, aisifiaye mvua...

MWANAMUZIKI wa BongoFleva, Amber Lulu, ameamua kuruka kama ndege kunguru, akisema watu wamuache kumhusisha kimapenzi na Uchebe.

Amber Lulu hivi karibuni aliweka ujumbe kwenye Insta Story akisema “Acheni Ujinga, mimi na Uchebe wapi na wapi mxiuuu” na kuibua mjadala mkali katika mtandao wa Istagram..

“Hayo ni mambo ya Instagram nimeshayazoea hayanipi shida pia sipendagi kuyaongelea, sijui hata yameanzia wapi na sina hata cha kuwaambia, hata nikisema niweke sawa suala hili wao itawasaidia nini kwanza hayo mambo ya Uchebe kamuulizeni Shilole,’ amesema.

## Vanesa in Dilema; Mwenda tezi na omo, marejeo ngamani

**Na Adam Fungamwango**

DUNIA ni duara. Nenda utakakokwenda. Zunguka utakavyozunguka, lakini siku moja utajikuta huenda umerejea kulekule ulikotoka. Hii ndiyo maana halisi ya methali ya ‘mwenda tezi na omo, marejeo ngamani’. Ni msemo wa kipwani, Maana yake ni kwamba utaenda mbele na nyuma ya tanga la baharini, pande hizo zote mbili zinaitwa tezi na omo, lakini marejeo yake ngamani, ikiwa na maana lazima tu mtu atarejea katikati ya tanga ambapo panaitwa ngamani.

Tujikite kwenye filamu yetu ya leo ambayo inashabihiana sana na msemo huu. Inaitwa ‘Vanesa in Dilema.’

Imechezwa na wasanii Rachel Haule aliyefariki 2014 jijini Dar es Salaam. Wengine ni Haji Adam, Simon Mwapagata na wengineo.

Inaanza kwa kuonyesha kwenye ofisi moja, kijana George anampenda mfanyakazi mwenzake aitwaye Vanesa.

Penzi linanoga na kuonekana kwa kila mtu. Nyuma ya pazia ya maisha ya Vanesa miaka mingi iliyopita ni kwamba alipewa mimba na mpenzi wake akiwa shuleni na mwanaume aliyekuwa akiitwa Jacob wakati wanasoma. Ilimfanya asimame shule na Jacob akakimbia mkono wa sheria.

Vanesa baada ya kujifungua, baadaye alijiendeleza na kuendelea na masomo hadi alipofaulu na kupata kazi mjini, iliyomkutanisha na George.

Vanesa furaha sasa inarudi kwa kukutana na mwanaume mwingine George. Siku moja aliamua kwenda kumtambulisha nyumbani kwao. Siku hiyo kaka yake kutoka Marekani alikuwa amewasili.

Wakati anatambulishwa kukazuka mshangao mkuu. Kumbe Vanesa anamfahamu kaka wa mpenzi wake. Ndiye Jacob. Vanesa anazirai. Kila kitu kinaanikwa wazi. Kumbe miaka mingi nyuma, Jacob ndiye alimpa mimba Vanesa shuleni na kukimbia, kabla ya kutimkia Marekani. Na mtoto mwenyewe yupo kijijini kwa bibi yake.

Ndugu wawili wakaingia kwenye bifu la kumgombea mwanamke mrembo Vanessa. Mwenyewe hajui la kufanya, ingawa alionekana kumpenda sana Jacob, yule aliyekuwa naye shuleni. Lakini kwa sasa anaishi na George. Hii ilimkera sana George. Kila wakati alikuwa akigombana na mwenzake.


Kukosa msimamo kwa Vanesa kulichochea uhasama na kuoaminika pande zote mbili, kiasi cha kila mmoja kuanza kuamua kumkwepa. Baadaye waliona ni bora wamalize ugomvi kila mmoja atafute mwanamke mwingine.

Sasa Vanesa akawa hapati mapenzi, au hapapatikiwi na yoyote kati ya wanaume hao wote wawili ndugu.

Akaanza kuona mabadiliko kwa kukosa upendo. Bahati mbaya sana, tayari alikuwa na ujauzito wa George, ambao mwanzo alitaka kwenda kuutoa ili tu awe na Jacob.

Jacob, anaamua kumuomba msamaha ndugu yake George na kumaliza bifu, huku akiaga kuwa anarejea nchini Marekani. Lakini akamshauri ndugu yake kumuoa Vanesa, kwa sababu anaujauzito wake, pia yeye mwenyewe ana mtoto kwake.

Baada ya kujishauri kwa muda mrefu, tena baada ya kuona Vanesa anapata tabu, George aliamua kumsamehe na kumuoa.





## Hawa wamewahi bwana!

**Na Adam Fungamwango**

WATU hawacheleweshi, yaani mwezi Septemba bado hata haujapambazuka vizuri, watu wameshatoa vitu vipya.

Tayari baadhi ya wasanii wameshatoa ngoma kali ambazo zimeanza kubamba kwenye mitandao ya kijamii na hata vyombo vya habari.

Hizi ni baadhi ya ngoma kali ambazo zimetoka mwanzoni tu mwa mwezi Septemba na kuzusha gumzo mitaani.

**NITAJARIBU-SALHA**

Hivi sasa kuna ingizo jipya la msanii wa kike aitwaye Salha. Yeye Septemba 2, ametoa ngoma yake aliyoiita ‘Nitajaribu’ Ni ngoma ya mapenzi na maudhui yake yanaonyesha jinsi msichana alivyoumizwa na mpenzi wake, hivyo anajaribu kujipoza kwa maneno ya faraja.

Anasema yeye hakopeshi wala hauzi, ila yeye ni wa kuumia kwa sababu akipenda anapenda mazima, akitekwa anatekwa mazima. Hata hivyo, ameumizwa kwenye mapenzi, ameachwa, hivyo anadhani kuwa wake yeye hajazaliwa.

**SINA NYOTA-MBOSSO**

Siku mbili baadaye, yaani Septemba 4, msanii maarufu nchini Mbosso, yeye alitambulisha ngoma yake iitwayo ‘Sina Nyota’.

Wimbo huu nao ni wa mapenzi. Ni yale yale tu malalamiko ya mtu anayeumizwa na mapenzi, lakini hii inaonekana kuwa pia tatizo lingine ni kipato kuwa kidogo.

**COCO-WILLY PAUL**


Huyu ni mmoja wa wasanii mwenye sauti nzuri na laini. Akimshirikisha Avril, ametoa ngoma yake Septemba 4 ambayo inaitwa ‘Coco’. Ni wimbo wa mapenzi pia. Lakini mapenzi haya ya hawa ni yale ya wale wanaoanza kupendana. Yanakuwa kama njiw a wanaofuatana wawili wawili. Wanaimba kwa kupokezana na kusifiana. Siku zote mwanzo wa mapenzi ni raha sana.

**NITACHELEWA-IBRAAH**

Septemba 5 ikatoka pini noja kali inayoitwa ‘Nitachelewa’. Imetolewa na msanii Ibraah na kuwa ni moja ya ngoma zilizotoka mapema mwezi huu na tayari zimeshaanza kuingia kwenye mioyo na ubongo wa mashabiki wa muziki wa bongo fleva nchini.

**NGONGINGO-RAYVANNY**

Inaonekana ni ngoma ambayo itafanya vizuri sana kutokana na maudhui ya wimbo yenyewe na staili yake. Nasema hivi kwa sababu Wabongo wanapenda sana muziki ambao unakuja na staili tofauti na waliozoea, kwenye maudhui na uimbaji pia. ‘Wowowo na ngongingo’ ni misemo ya miaka ‘90, hivyo inawakumbusha watu mbali. Hata aina yake ya uimbaji ni ile ya ucheshi, kutokana na Rayvanny kumshirikisha Baba Levo. Imetoka Septemba 6.



# Tyler jumba lake kufuru tupu

BILIONEA na staa wa filamu nchini Marekani, Tyler Perry, ameonyesha kwamba jarida la Forbes halikukosea kumtaja kama kuwa na ukwasi wa fedha, baada ya kuonyesha jumba lake jipya linalojengwa ambalo litakuwa na kiwanja binafsi cha ndege.

Kulingana na mtandao wa TMZ, nyumba hiyo ya kifahari itachukua eneo lenye ukubwa wa futi 35,000, sawa na heka 1,200.

Ujenzi wa nyumba hiyo tayari umeanza karibu na jiji la Atlanta, utajumuisha viwanja vya michezo, mabwawa makubwa ya kuogelea na kiwanja kikubwa cha kutua na kuruka ndege yake binafsi.



## Kumbe Burna Boy, Stefflon ni mke na mume?

MWIMBAJI nyota wa Nigeria, Burna Boy, na mpenzi wake ambaye ni rapa, Stefflon Don, inadaiwa wamefunga ndoa kwa siri.

Uvumi kwamba wawili hao wamefunga ndoa, unakuja baada ya Burna Boy, kuweka video fupi katika ukurasa wake wa Instagram, akionekana akimuita rapa huyo mke wake.

"Niangalie mke wangu," alisikika Burna Boy na kuendelea " "Unaona, unahitaji mke kama ninaye mimi, hili ni tatizo.

## Wanigeria kuwaburudisha Watanzania

WANAMUZIKI watatu kutoka Nigeria, watakwenda nchini Tanzania kwa ajili ya kutoa burudani katika shoo ya aina yake.

Wasanii hao ambao kila mmoja ana ngoma zake zimefanya vizuri duniani, ni Singahj, Joeboy na Wurld.

Shoo ambayo itawakutanisha wanamuziki hao kwa pamoja itafanyika Septemba 26 jijini Dar es Salaam.





## Vituko tupu talaka ya Dr Dre na mkewe

VITUKO vinazidi kujitokeza katika kesi ya talaka inayomhusu mwanamuziki mkongwe Dr Dre, na mkewe Nicole Young, baada ya mwanamama huyo kudai alipwe zaidi ya dola mlioni mbili kila mwezi kama ya matunzo ya watoto.

Mtandao wa PageSix, umedai katika maombi mapya waliyowasilishwa siku ya Alhamisi iliyopita, Young anataka Dre amlipe dola 1,936,399 kwa ajili ya kusaidia kuwatunza watoto wao.

Aidha, mkewe huyo amedai amekuwa na wakati mgumu wa kulipa bili mbalimbali ambazo alikuwa akipatiwa kwa miaka 24 ya ndoa yao, kutokana na Dre kuzuia kila kitu tangu kuanza kwa sakata hilo.

## Stella, Edeminokan si wanandoa tena

MWIGIZAJI mkongwe kutoka Nollywood, Stella Damasus na mumewe Daniel Ademinokan, inadaiwa wapo katika hatua ya mwisho ya kuachana baada ya kuishi katika ndoa kwa muda mrefu.

Kulingana na taarifa zilizopatikana, wanandoa hao wameshindwa kuondoa tofauti zao na sasa hakuna uamuzi mwingine watakaouchukua, bali hatua inayofuata ni kupeana talaka.

Stella na Ademinokan, tayari wamefuta kila kitu kinachowahusu katika akaunti zao za Instagram, jambo ambalo linaashiria shari imetawala kuliko heri.



MAKALA

# Hata lini simu zitaachwa ziendelee kuua abiria?



Dereva 'anachati' na kuendesha bila kujali madhara . **PICHA: MTANDAO.**

**Na Mwandishi Wetu**

MATUMIZI ya simu kwa madereva wa vyombo vya moto barabarani ni jambo linaloshuhudiwa kila siku na ajali nyingi zinaonekana zikisababishwa na kutumia simu.

Mara kadhaa wanaotumia simu huwagonga wenzao kwa nyuma, huparamia ukingo na wakati mwingine husababisha foleni na zogo barabarani.

Zogo hutokea pale wanapoendelea kusimama wakati magari yameruhusiwa . Matukio hayo hushuhudiwa kwa sababu madereva wahusika hawaangalii mbele kujua iwapo wameruhusiwa na taa au polisi, kwa sababu macho yao yameng'ang'ana na simu.

Mara nyingi madereva wanaowagonga wenzao kwa nyuma ni wale wanaotumia simu kuchati au 'kutongoa'. Wapo wengine wanaopanda ukingo wa barabara na kuanguka kisa, anachati.

Lakini, sharia zinazungumziaje kuhusu mazoea haya? Kama hapo ni wakati wa kufikiria jambo lolote ili kuokoa abiria, vyombo na miundombinu.

Ni muda mrefu sasa, imezoeleka dereva kutumia simu wakati ameshika usukani. Linakuwa kama jambo la kawaida licha ya kwamba ni kosa hata kama sharia hazikatazi.

Lakini, changamoto iliyoko leo ni wazi kuwa, siyo rahisi dereva kama walivyo Watanzania wengine, hawezi kuishi bila kuwa na simu. Lakini kwa upande mwingine iwapo ataendesha na kuzungumza na simu ni dhahiri madhara yake yanayojulikana.

Dereva hawezi kuacha kutumia simu kwa sababu ni chombo muhimu cha mawasiliano, lakini si lazima kukitumia wakati wote.

Suala hili linahusu maisha ya watu, kwa hiyo ni vyema sasa serikali au mamlaka ziamue cha kufanya kunusuru maisha ya wananchi, kwani Sheria ya Usalama Barabarani Sura ya 168 haijaweka kipengele cha kukataa kutumia simu dereva akiwa kwenye usukani.

Na ukweli ni kwamba, sheria husika haina kipengele chochote kinachopiga marufuku matumizi ya simu moja kwa moja, au kuweka 'head au ear phones 'masikioni na kuendesha gari, au hata dereva kuangalia video ndani ya gari awapo barabarani.

Sheria ya Usalama Barabarani ilitungwa mwaka 1973, na kufanyiwa marekebisho ya mara kwa mara ya mwisho, yakifanyika 1996 na sasa yanasubiriwa yafanyike mengine kuhusu matumizi ya simu.

Kwa upande mwingine Mamlaka ya Udhibiti wa Usafirishaji wa Nchi Kavu (LATRA) kanani zake za mwaka 2007 zinakataza matumizi ya simu wakati dereva anaendesha. LATRA ambayo awali ilikuwa SUMATRA kanuni za usafirishaji abiria za mwaka 2007, kanuni ya 18(1)(i) inakataza dereva kuendesha gari wakati anatumia simu.

Kwa hiyo ni makosa kwa mujibu wa kanuni za LATRA, dereva wa daladala na basi la masafa la abiria yakiwamo ya wanafunzi kutumia simu za mikononi , kuweka 'head au ear phones' wakati yuko barabarani na wasafiri ndani ya chombo? Jibu ni hapana. Kwa sababu siyo sharia ya Usalama Barabarani inayokataza. .

Aidha, kanuni za Leseni ya Usafirishaji wa Magari ya Mizigo za mwaka 2012, zinakataza dereva wa gari la shehena kutumia simu au kifaa kinachofanana na hicho wakati wa kuendesha lori la mizigo . Hata hivyo kanuni hizo hazina nguvu kwa kila dereva kwa sababu zinawahusu madereva waliopewa leseni na SUMATRA au LATRA wakati huu.

Zama hizi leseni za kuendesha hutolewa na Mamlaka ya Mapato (TRA). Lakini cha msingi ni Sheria ya Usalama Barabarani, irekebishwe kukataza matumizi ya simu barabarani. Mara ya mwisho sharia hiyo ilirekebishwa mwaka 1996 na sasa ni wakati wa kuiangalia, ili kujali usalama na maisha ya watu.

Suala la kutumia simu limeachwa kwa askari wa usalama barabarani, kuamua kuhusu matumizi yake wakati wa kuendesha gari. Kifungu cha 42(c) cha Sheria ya Usalama Barabarani kinasema, askari wanaweza kutoa tafsiri kuhusu kifungu hicho kuangalia na kufanya maamuzi ya kutumia simu wakati wa kuendesha gari.

Polisi ndiyo wanaoweza kusema ni uendeshaji wa hatari au wa kipuuzi. Lakini hakujawa na katazo kisheria la moja kwa moja.

Kuna haja ya watunga sheria wakati huo, kujiongeza kiteknolojia kwenye matumizi ya simu ya mkononi, ili kukabiliana na changamoto hiyo, ambayo inachangia ajali nyingi za barabarani.

Pengine kuna haja yakufanyika marekebisho na kuweka katazo la kutumia simu za mkononi kwa madereva, wakiwa wanaendesha chombo cha moto.

Iwe basi la abiria, gari binafsi, pikipiki, baiskeli, lori la shehena na treni. Iwe ni katazo la kisheria ili kuipa nguvu zaidi.

Licha ya kwamba asasi za kiraia kama Chama cha Wanahabari Wanawake (TAMWA), zimekuwa zikisisitiza sharia hiyo kubadilishwa, ili kuweka adhabu kali na kupiga marufuku ulevi na kukataza kilevi kwa madereva kwani ni chanzo cha ajali hizo, bila shaka kuna haja ya kuongeza kipengele kukatazwa madereva kuongea na simu wakiendesha chombo cha moto.

Itangazwe kisheria kuwa ni kosa la jinai na ziandaliwe kanuni na adhabu kwa yeyote atakayepatikana na hatia ya kuendesha na kutumia simu.

Mataifa yaliyoendelea kwa mfano nchi za Ulaya, madereva wanaruhusiwa kuendesha wakizungumza na simu . Sheria zao zinawaruhusu kutumia simu, lakini si kuishika mkononi. Pengine aongee kwa kutumia kitu wanachokiita 'handheld device'.

Lakini, kwa magari ya abiria sharia zinakataza ni lazima dereva aegeshe gari pembeni tena eneo lenye usalama ashuke, ndipo aanze kuzungumza na simu.

Pengine huu ndiyo wakati wa Tanzania kupata mwongozo washeria na abiria kufumbua macho kuhusu usalama wao wanapoendeshwa na dereva anayeongea na simu, wakati huo huo anaendesha chombo cha moto kiwe daladala, basi la masafa, lori la shehena na mwendo wa haraka.

Sivyo tu, hata pikipiki au teksi na bajaji. Simu ni hatari kwa uendeshaji magari barabarani kwa dereva, abiria, watumia miguu, miundombinu na mazingira.

# AFRIKA YANUSA WTO

## ■Wagombea wake watatu wapitishwa
## ■Kenya, Nigeria, Misri watoana jasho

**Na Mwandishi Wetu**

AFRIKA imepewa nafasi ya kipekee kwa kuingiza wagombea watatu kati ya wanane, wanaowania kuongoza Shirika la Biashara Duniani (WTO).

Tangu kuanzishwa kwa shirika hilo, hakuna Mwafrika aliyepata nafasi ya kuwa Mkurugenzi Mkuu, hivyo ni nafasi nzuri kuonyesha tofauti endapo mmoja wao atachaguliwa.

Wagombea wa Afrika ambao majina yao yamepitishwa katika kinyang'anyiro hicho ni Ngozi Okonjo-Iweala wa Nigeria, Amina Mohamed wa Kenya na Abdel-Hamid Mamdouh kutoka Misri.

Uchaguzi huo unavuta hisia kati ya wanadiplomasia wa Kiafrika, ambao wanataka kuona mtu kutoka bara hilo anaingia kwenye uongozi wa juu katika shirika hilo.

Kati ya, Ngozi, Amina na Abdel-Hamid, mmoja wao akishinda kwenye mchakato wa uchaguzi, bara la Afrika litajivunia kuwa na mtu wake.

Kazi ya WTO ni kuweka sheria za biashara ulimwenguni na kutatua mizozo ya kibiashara kati ya mataifa wanachama.

Shirika hilo ambalo makao yake makuu yako Geneva, Uswiss, pia linaweka kanuni na misingi kwa kila nchi ambazo zimesaini.

Mkurugenzi mkuu pamoja na kazi zingine, anahudhuria mikutano ya nchi tajiri duniani za G20 na G7, pia anaweza kutekeleza makubaliano yaliyofikiwa kati ya viongozi wa nchi mbalimbali.

Ingawa, Mkurugenzi Mkuu jukumu lake ni usimamizi peee, lakini endapo kiongozi huyo atatoka Afrika anaweza kusaidia kuhakikisha masilahi ya bara yanazingatiwa katika shughuli za WTO.

Mategemeo ni kuona kutakuwa na unafuu kutoka kwa wenye viwanda, wafanyibiashara ambao wanavuka mpaka kununua bidhaa hadi kwa mnunuzi wa hali ya chini wanapata nafuu.

Barani Afrika, biashara inaonekana ndio nguzo muhimu inayosababisha ukuaji wa uchumi na maendeleo endelevu katika kupambana na umasikini.

"Misaada kutoka nje haitafaidi Afrika. Ni biashara pekee itakayoonemesha kama mahali pengine popote," anasema David Luke, mkuu wa kituo cha sera za biashara katika Tume ya Uchumi ya UN ya Afrika.

" Waafrika wa kawaida wataelewa pale mwafrika mwenzao akiongoza WTO na kuonyesha tunazingatia usawa wa biashara."

Bi Okonjo- Iweala ameliambia Shirika la Utangazaji la Uingereza (BBC) kuwa, katika sera zake anajali zaidi mwafrika wa kawaida.

"Nataka kujua namna wanawake na vijana, ambao wako nyuma ya injini za ukuaji barani Afrika, wanafaidika na biashara ya ulimwengu".anasema Okonjo. CHANZO CHA PICHA,GETTY IMAGES



Wagombea wa nafasi ya Mkurugenzi Mkuu wa Shirika la Biashara Duniani (WTO), kutoka kushoto Amina Mohamed wa Kenya, Ngozi Okonjo-Iweala wa Nigeria na Abdel-Hamid Mamdouh kutoka Misri.

Nia yake ni kuona Afrika inaondokana na biashara ya kusafirisha malighafi, badala yake ni lazima kuanza kujishughulisha na uongezaji thamani kwa bidhaa zake ili kushindana katika soko la kimataifa.

Anasema, kwa mfano, asilimia 94 ya dawa kwenye bara hilo zinatoka nje, wakati tunaweza kuzalisha hapa Afrika.

Amina kwa upande wake, ambaye amewahi kuwa waziri wa biashara na mambo ya nje wa Kenya, anasema anaweza kuleta mtazamo mpya ambao ulikuwa unahitajika tangu zamani.

Hata hivyo, mgombea huyo hakutaka kuhukumiwa katika kuonekana kama kiongozi mwenye fikra za Pan Afrika, lakini anajipambanua kuwa yeye atakuwa kama kiongozi mzoefu na mjenzi wa makubaliano.

Mamdouh, ambaye amekuwa mwakilishi wa siku nyingi wa Misri tangu mwaka wa 1985, anasema uzoefu wake katika shirika hilo, utamwezesha kuona jinsi gani anaweza kulisaidia bara la Afrika na watu wake.

"Ajenda yangu kwa Afrika itakuwa kuwajumuisha watu wote katika mfumo wa biashara," anaisema.

Anaongeza kwa kueleza "Pia nitatoa wito kwa viongozi wa kisiasa katika nchi za kiafrika kuzifuata sera zao za kibiashara."

Pamoja na matumaini ya wagombea hao kutaka kunyanyua bara la Afrika kibiashara, lakini wanaweza kumkwamisha kutokana na nafasi hiyo ya WTO anaweza kushawishi marais, lakini hawezi kuwalazimisha kufanya kile anachotaka.




Jengo la makao makuu ya WTO

Mkataba wa Biashara Huria ndani ya Afrika (AfCTA), kiongozi wa shirika hilo anaweza kuingilia na kutoa uamuzi.

Makubaliano hayo ambayo utekelezwaji wake umeahirishwa kutokana na janga la virusi vya covid- 19, unatarajia kuanzisha eneo kubwa zaidi la biashara huria duniani.

"Hii itahakikisha bidhaa za hali ya juu zinazalishwa kutoka bara, na hivyo, itasaidia kuongezeka kwa kipato kwa watu na kusaidia kutokomeza umaskini wa muda mrefu," anasema Luke ambaye ni mtaalamu wa biashara.

Sheria na malengo ya AFCTA yanaambatana na yale ya WTO, hivyo kama kiongozi wa kiafrika ataongoza shirika hilo la biashara anaweza kusaidia kuielekeza misaada kwa bara hilo.

Katika nafasi hiyo, anaweza kuongoza kutoa msaada ya kiufundi, uchambuzi wa biashara, utaalamu wa sera, na kuleta ndoto ya biashara huria.

Hata hivyo, wakati jicho na matumaini ya Waafrika kuona wanaoongoza shirika hilo, kuna ongezeko la matamshi yenye kuegemea kujilinda binafsi kwa viongozi wa mataifa tajiri duniani.

Vita vya biashara kati ya Marekani na China, na sera za Rais wa Marekani Donald Trump za kutekeleza mfumo wa kuipa kipau mbele dhidi ya marafiki zake wa kibiashara, zinaonekana kugeuza wimbi dhidi ya imani ya biashara huria.

Vikwazo vilivyowekwa kwa sababu ya kukabili maambukizi ya virusi vya corona, pia vimeathiri harakati ya usafirishaji huduma na bidhaa muhimu kwa wanaozihitaji.

**HOFU YATANDA**

HOFU ya Marekani kukataa kuidhinisha uteuzi au kuteuliwa kwa viongozi na majaji wa WTO, ambao wanaosimamia rufaa dhidi ya maamuzi ya shirika hilo, imeweka katika hali ya sintofahamu kuhusu mchakato huo.

Hali hiyo inatishia kudhoofisha shirika hilo kwa jumla. Pia kuanzisha sheria mpya zenye misingi ya usawa kwa nchi zote, imekuwa changamoto nyingie.

Mwaka wa 2001, WTO ilizindua mazungumzo yanayoitwa "Mazungumzo ya Doha", ambayo yalitakiwa kuandaa mipangilio mipya ya kusaidia mataifa yanayoendelea.

Karibia miongo miwili, mazungumzo hayaleta matunda, hivyo kiongozi mpya anayetarajiwa kupatikana Novemba utakuwa mtihani wake wa kwanza.

# Jino la Lumumba sasa kurudishwa nyumbani

**BRUSSELS, Ubelgiji**

MAHAKA moja nchini Ubelgiji, imeamuru kurudishwa jino la Waziri Mkuu wa zamani wa DRC, Patrice Lumumba, ambalo lilichukuliwa baada ya kuuawa miezi michache baada ya nchi hiyo kupata uhuru.

Jaji aliyetoa uamuzi huo, aliamuru jino hilo kukabidhiwa familia yake.

Lumumba aliyekuwa waziri mkuu wa Congo baada ya kujipatia uhuru kutoka kwa Ubelgiji 1960, aliuawa mwaka 1961 baada ya kutekwa na wapiganaji waliotaka kujitenga.

Serikali ya Ubelgiji ilihusika katika kifo chake na mwaka 2002 iliomba msamaha rasmi. Jino la Lumumba lilichukuliwa na ofisa mmoja wa polisi wa Ubelgiji ambaye alisaidia kuuzika mwili wake, na baadaye serikali ya Ubelgiji ililichukua na kulihifadhi.

Mahakama hiyo, ilisema jino hilo sasa linafaa kupewa mtoto wa kike wa Lumumba, Juliana Lumumba , ambaye aliandika barua kwa mfalme wa Ubelgiji akiomba lirudishwe. Uliripoti mtandao wa Brussels Times.

Kulingana na mtandao huo, uamuzi huo uliotolewa siku ya Alhamisi wiki iliyopita, unafuatia uamuzi mwengine wa ofisi ya kiongozi wa mashtaka wa jimbo ambaye alitaka mabaki ya Lumumba kurudishwa kwa familia yake.

Familia yake imepongeza hukumu hiyo wakisema ni hatua nzuri ya kutambua utu wa kiongozi huyo.

Mpwa wake Jean Lumumba alisema familia yake haikumzika ndugu yao kwa sababu mwili wake uliyeyushwa kwa tindikali.

**BBC.**



Kiongozi wa Korea Kaskazini, Kim Jong Un, akishiriki jaribio la urushwaji wa kombora la kisasa zaidi la masafa marefu. Picha hiyo ilitolewa juzi na shirika la habari la nchi hiyo (KCNA).**(PICHA: REUTERS)**

# Mabaki ya samaki 'Mafishi' yaibwa

**LUSAKA, Zambia**

MABAKI ya samaki maarufu kwa jina la 'Mafishi'nchini Zambia, ambaye kifo chake kiliombolezwa na wananchi wa Zambia, yameibwa na watu wasiojulikana.

Mabaki ya 'Mafishi' yaligundulika yametoweka katika sehemu yalipohifadhiwa katika Chuo Kikuu cha Copperbelt (CBU), mjini Lusaka.

Samaki huyo ambaye aliishi kwenye kidimbwi cha maji ndani ya Chuo hicho kwa zaidi ya mwongo mmoja na wanafunzi walimchukulia kama chanzo chao cha bahati.

Kifo cha samaki hiyo, kiliombolezwa na viongozi wakuu serikalini, akiwamo Rais Edgar Lungu na baadhi ya mawaziri wake.

Gazeti la Zambia Daily Mail, lilimnukuu Naibu Mkuu wa chuo hicho, Naison Ngoma, akithibitisha kutoweka kwa mabaki hayo na kueleza uchunguzi umeanzishwa kubaini kilichotokea.

"Nilifahamishwa kwamba samaki huyo alianza kutoa harufu mbaya kwenye jokofu, Iakini nilipouliza yuko wapi niliambiwa ametoweka"alisema.

Prof. Ngoma alisema huenda samaki huyo ameliwa au kutupwa.

Alisisitiza ripoti ya uchunguzi huo ikitolewa, hatua za kinidhamu zitachukuliwa dhidi ya wale wote waliohusika kwa kutoweka kwa mabaki ya samaki huyo.

**BBC**

# Uingereza yakataa kubatilisha muswada

**LONDON, Uingereza**

UMOJA wa Ulaya (EU) umeonya muswada mpya wa Uingereza kuhusu biashara utakuwa moja ya ukiukaji wa mpango wa Brexit.

Kauli hiyo imetolewa baada ya kufanyika kwa mkutano wa dharura kati ya Umoja huo na Uingereza, mazungumzo ambayo yameonekana kukwama.

Uingereza inataka kuidhinisha muswada wa Soko la Ndani, ambao utaweza kuipa nguvu za kuubadilisha mpango wa Brexit ambao umeharibu kwa kiasi kikubwa uaminifu kati ya pande hizo.

Miongoni mwa maswala mengine, Umoja wa Ulaya unadai muswada huo mpya utahujumu kile kinachojulikana kama makubaliano ya 'Ijumaa Njema' ambayo yalimaliza miongo kadhaa ya machafuko Ireland Kaskazini.

# Nchi 10 kuwachukua watoto 400

NCHI 10 za Ulaya zimekubali kuwahifadhi watoto 400 walionusurika katika ajali ya moto iliyotokea ndani ya kambi ya wakimbizi ya Moria.

Waziri wa Mambo ya Ndani wa Ujerumani, Horst Seehorfer, alisema nchi hizo wanachama wa Umoja wa Ulaya, zimekubali kuwachukua watoto hao wadogo ambao hawana wazazi wala jamaa katika kambi hiyo.

Ujerumani na Ufaransa zitachukua idadi kubwa ya watoto hao, kila nchi ikijitolea kuwachukua 100 hadi 150.

Maelfu ya waomba hifadhi wamelala nje kwa usiku wa tatu mfululizo kwenye kisiwa cha Lesbos, baada ya kambi hiyo kubwa ya wahamiaji kuteketea kwa moto.

Polisi walifika jana katika eneo hilo kulinda usalama, huku wengine wakiwazuia wahamiaji wasifike katika bandari ya karibu.

# Urusi yataka kumhoji Navalny hospitalini

**MOSCOW, Urusi**

URUSI imesema inapanga kumhoji kiongozi wa upinzani Alexei Navalny anayetibiwa nchini Ujerumani, baada ya serikali kupuuza madai ya kuhusika na kumpa sumu.

Ujerumani ilidai ina uthibitisho kwa kiongozi hiyo alipewa sumu aina ya Novichok, inayoathiri mishipa ya fahamu.

Polisi wa Urusi ilisema kufuatia ripoti kuwa Navalny, ameanza kupata fahamu, huenda watahitaji kumuhoji kuhusu ufafanuzi, wakiwa pamoja na wenzao wa Ujerumani.

Serikali ya Urusi inapinga majaribio yoyote ya kuilaumu kwa tukio hilo la sumu, ikisisitiza inataka kujua nini kilitokea.

**DW**

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

## VIWANJA/MASHAMBA

**KIWANJA KINAUZWA,** Kiwanja cha Biashara kinauzwa Regent Estate Dsm mita za mraba 1300. Piga; 0693 689996, 0757 129546.

NIPASHE NI JIBU LAKO
NJOO UTANGAZE NASI
KWA BEI NAFUU SANA
Tutumie E-mail: advertise@guardian.co.tz, au piga simu: 0782253676

## KUPOTEA KWA CHETI



115897402

**Ladislaus U. Philiph** anatangaza kupotea kwa cheti cha kidato cha nne chenye **index namba S0795-0085** kilichotolewa na Baraza la Mithiani la Taifa Tanzania mwaka 2006 katika shule ya Sekondari Kisale. Yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo chochote cha Polisi. Polisi Taarifa: **SAM/B1/24/VOL.XIV/24**

## KUPOTEA KWA CHETI



115897502

**LOVENESS CHARLES MBISE** anatangaza kupotea kwa cheti cha kidato cha nne chenye **index namba S.0214/0059** kilichotolewa na Baraza la Mitihani la Taifa kupitia MSALATO SEKONDARI mwaka 2016. Yeyote atakayekiona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya polisi: **DAR/CHU/RB/658435/2020.**

## KUPOTEA KWA CHETI



115897102

**ELIBARIKI LUKUMAI ABRAHAM** anatangaza kupotea kwa cheti cha kidato cha nne chenye index namba **S.1589-0059** kilichotolewa na Baraza la Mitihani la Taifa kupitia MWANZA BAPTIST SEKONDARI mwaka 2011. Yeyote atakayekiona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya polisi: **KLR/RB/3782/2018.**

## KUPOTELEWA NA KADI YA PIKIPIKI

**JUMA KAYAKOSA KAYOMBO** anatangaza kupotelewa na kadi ya pikipiki aina ya **TBETTER** yenye chassis namba **LZEPCKLA3C6816080** egine namba **ZJI62FMJC2516199.** Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi kilicho karibu. Taarifa ya polisi **MBE/MBE/RB/649202/2020.**

115897302

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**HAMIS ABDALA MPONJO** ANATANGAZA KUPOTELEWA NA KADI YA GARI AINA YA **MITSUBISH FUSO** YENYE NAMBA ZA USAJILI **T 737 CSA.** Chassis namba **FK41J550842.** Engine namba **6D17FE6913.** YOYOTE ATAKAYE IONA ATOE TAARIFA KITUO CHOCHOTE CHA POLISI. TAARIFA YA POLISI: **DAR/CEN/RB/657712/2020.**

115896702

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA**

**USIMAMIZI WA MIRATHI**

**(S.M.M.1984 NYONGEZA YA 5 KANUNI YA 2)**

**Katika mahakama ya mwanzo DODOMA MJINI**

**Usimamizi wa mirathi 81/2020**

**Ombi la YASINI SWEDY MUSSA kuteuliwa Msimamizi wa mirathi ya Marehemu SWEDY MUSSA SWEDY**

Watu wote wanaodaiwa kuwa na uhusiano wowote na Mirathi ya Marehemu huyo wanaalikwa kuja na kuhudhuria Shauri wakitaka mnamo tarehe 17/09/2020 kabla huyo mwombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa Mirathi hiyo. Tarehe 01/9/2020

HAKIMU
MAHAKAMA YA MWANZO
CHAMWINO MJINI
DODOMA.

215897602

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA**

**USIMAMIZI WA MIRATHI FORM 11**
**(S.M.M.1984 NYONGEZA YA 5 KANUNI 2)**

**Katika mahakama ya mwanzo DODOMA MJINI**

**Usimamizi wa Mirathi 116/2020.**

**Ombi la GRACE CHARLES MTOWA kuteuliwa Msimamizi wa Mirathi Marehemu BLANDINA CHARLES MTOWA**

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote na Mirathi ya Marehemu huyo wanaalikwa kuja na kuhudhuria kesi wakitaka mnamo tarehe 05/10/2020 kabla huyo mwombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa Mirathi hiyo.
Wosia wa marehemu huyo upo mahakamani waweza kukaguliwa. Tarehe 10/9/2020.

Sahihi
PRINCIPAL
PRIMARY COURT MAGISTRATE
URBAN DODOMA

215897702

**THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA**
**JUDICIARY**

**IN THE DISTRICT COURT OF SENGEREMA**
**AT SENGEREMA**

**CIVIL CASE NO 8 OF 2020**

**JOSEPH BOYA KACHILE ..................PLAINTIFF(S)**

**versus**

**CHRISTOPHER STEVEN...................... DEFENDANT(S)**
**SUMMONS TO FILE WRITTEN STATEMENT OF DEFENCE**
**O.V,r1 CPC**

**TO: CHRISTOPHER STEVEN**
WHERE the above named plaintiff(s) has/ have instituted a suit against you upon the claim the particular of which are set out in annexed copy of the plaint;
**YOUR ARE HEREBY NOTIFIED** that you must file your **WRITTEN STATEMENT OF DEFENCE** in duplicate within twenty one (21) days of service of this notice upon you. if there is more than one plaintiff, additional copies of your written statement of defence, must be file sufficient for service on each of the plaintiffs. if there are more defendants than one each of the other defendants.
**AND TAKE NOTICE** that the case also has been fixed for order before Hon A.J KYAMBA magistrate on the 21 day of SEPT 2020 at SENGEREMA 08:30 O'clock in the forenoon/afternoon.
**GIVEN UNDER MY HAND AND THE SEAL OF THE COURT this.... 31ST of AUGUST 2020**

REGISTRAR/MAGISTRATE
the receipt of a duplicate of this summons this ..... day
DEFENDANT

115897802

Uza,
Chenye Thamani
Kubwa Kwa Kutangaza
Nasi Kwa Bei Poa
Tupigie 0782253676

Kwa Habari Motomoto
usikose Gazeti lako
la Nipashe kila siku
Tupigie
0782253676
Nipashe
www.ippmedia.com
MWANGA WA JAMII

TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

HADITHI

# HADITHI

ILISEMWA hapo zamani kuwa dunia inaharibiwa na vitu viwili tu. Mapenzi na mali. Vitu hivi vinaweza kumfanya binadamu aende popote, afanye chochote kile ili awenavyo, wengine wanakwenda mbali zaidi mpaka ikiwezekana hata kutoa uhai wa wenzao.

Shani, binti wa kitajiri anapitia kwenye mikasa mikubwa mizito ya kupotezwa kwa wazazi wake na kumsababishia ukiwa na mawazo tele. Wakati ikionekana binti huyo pekee kwa wazazi wake akielekea kurithi utajiri wa wazazi wake, kiu ya damu inaanza kuwaingia baadhi ya ndugu za wazazi wake ili apoteze maisha, wao waweze kumiliki mali hizo. Hapo ndipo uhai wa Shani unapokuwa matatani na patashika nguo kuchanika inapoanza. Fuatilia mkasa huu kuburudisha, kuelimisha na kusikitisha.

# Mauaji Harusini-29

**Mtunzi anapatikana (0716 350534)**


**Na Adam Fungamwango**

***ILISEMWA hapo zamani kuwa dunia inaharibiwa na vitu viwili tu. Mapenzi na mali. Vitu hivi vinaweza kumfanya binadamu aende popote. Afanye chochote kile ili awe navyo, wengine wanakwenda mbali zaidi mpaka ikiwezekana hata kutoa uhai wa wenzao.***

***Shani, binti wa kitajiri anapitia kwenye mikasa mikubwa mizito ya kupotezwa kwa wazazi wake na kumsababishia ukiwa na mawazo tele.***

***Wakati ikionekana binti huyo pekee kwa wazazi wake akielekea kurithi utajiri wa wazazi wake, kiu ya damu inaanza kuwaingia baadhi ya ndugu za wazazi wake ili apoteze maisha, wao waweze kumiliki mali hizo.***

***Hapo ndipo uhai wa Shani unapokuwa matatani na patashika nguo kuchanika inapoanza. Fuatilia mkasa huu kuburudisha, kuelimisha na kusikitisha.***




MAELEZO ya Shani alianza kumpa wasiwasi Eddy. Kama mwenyewe ameshaanza kugundua kuwa ndugu zake wanamtenga, au hawamchangamkii tena kama zamani, je mioyo ya baba zake wadogo ikoje?

Alianza kuunganisha matukio. Hivi ni kweli baba zake wadogo wanaweza kukubali msichana mdogo kama yule kurithi mali zote? Lakini si walishaambiwa zingine watapewa? Inawezekana hawakuridhika.

Ni nini hawa ndugu wanachofikiria kwa msichana huyu? Je, tukio la chakula kile cha sumu alichotaka kuwekewa siku ile na marehemu Fikiri lina uhusiano ya jambo hili?

Iwe ni baba zake wadogo, au watu wengine, lakini ni ukweli usiopingika kuwa Shani alikuwa anawindwa ili auawe. Hilo Eddy alilitambua vema.

Na ndiyo maana baada ya jana yake kulala naye mpaka asubuhi, alimshauri aliache gari lake pale nyumbani kwake na Eddy kumtaka kupanda gari lake aina ya Toyota Brevis, akimpeleka ofisini.

Ndani ya gari, kuna vitu kadhaa ambavyo Eddy alimshauri Shani aachane navyo na pia kurekebisha mwenendo wa vitu ambavyo amekuwa akivifanya au kwenda kula siku, ili kuepuka maadui ambayo wanaweza kuwa wanamfuatilia. Alikubali kufuata, ingawa yeye hakudhani kama yuko kwenye hatari kubwa kiasi hicho. Ni Eddy pekee aliyejua kuwa Shani alikuwa hatarini, lakini hakutaka kumwambia ili kutomtisha.

Kwa jinsi alivyokuwa akimweleza, Shani alimshangaa Eddy kwa kuona ana uwezo na upeo mkubwa wa mambo ua kiitelejensia kama vile askari mpelelezi.

**Alijiambia mwenyewe akiwa ofisini baadaye kuteremshwa na gari, huku na yeye akielekea ofisini. Shani pia hakujua kuwa Eddy alikuwa anafanya kazi wapi. Alichotambua kwa kuambiwa na mwenyewe kuwa ni mchakarikaji tu wa mjini maarufu kama 'mesheni tauni'.**

Hata hivyo Eddy alivyokuwa akimwambia ni yale mambo ya msingi tu na si ya ndani.

Vyote hivyo vilimfanya Shani azidi kumpenda Eddy na kujiona mwenye bahati kubwa kupata mtu wa aina ile.

"Huyu ndiye mlinzi wangu, huyu ndiye mtu niliyekuwa namhitaji kwenye maisha yangu. Huyu ndiye mpenzi niliyemtaka. Na huyu ndiye nataka awe mume wangu." Alijiambia mwenyewe akiwa ofisini baadaye kuteremshwa na gari, huku na yeye akielekea ofisini. Shani pia hakujua kuwa Eddy alikuwa anafanya kazi wapi. Alichotambua kwa kuambiwa na mwenyewe kuwa ni mchakarikaji tu wa mjini maarufu kama 'mesheni tauni'.

*********************************

Kitu kilichompa faraja kidogo Eddy ni kujua kuwa yoyote aliye nyuma ya mpango wa kumuua Shani, tayari alishajua kuwa mipango imeenda kama ilivyopangwa.

Wanachosubiri tu ni Shani kufa, na ndiyo maana walimuua Fikiri kwa kudhani kuwa tayari ameshamaliza kazi waliyomtuma.

Ni kipindi ambacho watakuwa wanasubiria matokeo, Eddy aliamua kukitumia kufanya upelelezi wake mdogo, bila kuhusisha ofisi yake.

Alijua ofisini hawawezi kukubali afanye kazi ndogo kama hiyo ambayo pia hawana uhakika nayo.

Kazi ya kuchunguza nani aliyempa sumu marehemu Fikiri kuweka kwenye chakula cha msichana Shani.

Halafu hapo hapo siku chache baadaye aliyebambwa na sumu hiyo naye anauawa, ni kazi ya polisi wa kawaida, siyo mtu kama yeye ambaye amefuzu kwenye nyanja za juu zaidi za kipelelezi.

Hivyo alichotaka kufanya ni kuipeleleza kimya kimya bila yoyote kujua. Lengo ni kutaka tu kujua ni nani anayefanya vitendo hivi, ili tu akusanye ushahidi wa kumtia kwenye mikono ya polisi.

Ilipotimu jioni alimpitia kwenye ofisi yake iliyopo maeneo ya Posta jijini Dar es Salaam na kumrejesha nyumbani wake Ununio.

"Kuanzia leo mimi ndiyo nitakuwa dereva wako. Lile gari lako litaendelea kukaa pale hadi hapo nitakapokwambia vinginevyo. Sawa?"

Sura ya Eddy ilionekana kubadilika. Mara nyingi akiongea maneno yenye mlengo ya kipelelezi, huwa hata sura yake inabadilika kiasi fulani.

Shani aliligundua hilo. Ndiyo maana wakati mwingine anamuona kama ni mtu wa ajabu kidogo.

"Sawa dereva, usiwe na wasiwasi, na ikifika mwisho wa mwezi nikumbushe mshahara wako." Shani alizungumza kwa mzaha. Mzaha ambao ulimlainisha Eddy kutoka kwenye sura yake kikazi, na kurejea ile ya kawaida iliyozoeleka sana. Shani alifanya vile kwa makusudi ili kumuondoa kwenye hali ile.

Alijua kuwa mara nyingi Eddy ni mtu wa maneno ya mapenzi, mzaha, utani na ni kama komediani fulani hivi. Lakini cha ajabu kuna wakati anageuka na kuwa kama askari fulani hivi.

"Kwa wewe sitaki mshahara wa pesa, najua unazo tu, utanilipa." Alidakia Eddy.

"Sasa unataka nikulipe nini ambapo sina?"

Jibu hilo lilimfanya Eddy aangue kicheko.

"Mhh Shani siku hizi na wewe hujambo kwa maneno."

"Si umenifundisha mwenyewe."

"Na kweli. Tena vya kufundishwa huwa vinazidi,"

"Kweli kabisa."

"Sasa wewe ulitaka nikulipe nini?" Shani alirudi swali.

"Unilipe wewe." Ni jibu lililowafanya wapenzi hao wapya waange vicheko.

"Yaani Eddy wewe, sijakupatia mwezio, unajua wewe una vituko?"

"Kwani wewe uliponiuliza hilo swali, utarajia nikujibu nini?"

"Kwa hiyo nikulipe mimi."

"Wewe ndiyo."

"Haya nitakulipa."

"Hayo ndiyo maneno."

Alipomshusha kwake, Eddy alirudi nyumbani kwake Kijitonyama.

Hata hivyo akili yake ilimwambia kuwa itafika wakati itabidi awe naye.

Awe naye kama mpenzi wake, lakini pia ni kwa ajili ya ulinzi wake pia.

Aliwaza jinsi Shani alivyo mwenye furaha sana kwa sasa kwa ajili yake.

Na pia hajui chochote kuhusu kuwepo kwenye hatari. Hicho ndicho alichokuwa akikitaka Eddy.

Hakupenda msichana huyo aishi kwa hofu. Kuishi kiitelejensia awaachie wao kina Eddy.

**ITAENDELEA JUMAMOSI**

# DYABALA KUPEWA MIAKA MITANO JUVENTUS




**TURIN,** Italia

KLABU ya Juventus ina mpango wa kumpa mkataba mpya wa miaka mitano, Paulo Dybala.

Mkataba wa awali ya Dybala ndani ya Juventus unatarajiwa kumalizika Juni 2022 baada ya kuusaini mwaka 2017.

Juventus wanataka kumuongeza straika huyo mkataba kutokana na ubora ndani ya timu hiyo na amekuwa kati ya wachezaji tegemeo.

Dybala ambaye msimu uliopita aliibuka kuwa mchezaji bora ndani ya Serie A, pia aliisaidia timu hiyo kutwaa ubingwa wa Ligi Kuu na kuifikisha timu yake hatua ya 16-Bora ya Ligi ya Mabingwa Ulaya.

Ripoti zinaeleza kuwa, Mkurugenzi wa Ufundi wa Juventus, Fabio Paratici yupo kwenye mazungumzo na wakala wa Dybala Jorge Antun kwa ajili ya mkataba mpya.

Uongozi wa klabu hiyo una mpango wa kumpa mkataba wa miaka mitano kwa maana hiyo Dybala atakuwa ni mchezaji wa pili kulipwa vizuri ndani ya kikosi hicho baada ya Cristiano Ronaldo.

Dybala atakuwa analipwa kiasi cha euro milioni saba kwa msimu na euro milioni 10 kama bonasi ndani ya kikosi hicho.

Juventus inataka kukamilisha dili hilo baada ya Klabu za Man United, PSG na Real Madrid kuonekana kusaka saini ya mchezaji huyo.

# Klopp azungumzia usajili wa Liverpool

**LIVERPOOL,** England

KOCHA wa Liverpool, Jurgen Klopp amesema klabu yake haiwezi kufanya usajili kama washindani wao wanavyofanya, kwani klabu zinatofautiana kuanzia umiliki na mikakati.

Mabingwa hao watetezi wa Ligi Kuu nchini England, hadi sasa wamefanya usajili wa mchezaji mmoja tu ambaye ni Kostas Tsimikas kwa dau la pauni milioni 11.7 wakati wapinzani wao kama Chelsea tayari wametumia zaidi ya pauni milioni 200.

Klopp amesema uwapo wa janga la virusi vya corona umetengeneza utofauti wa kiuchumi baina ya klabu wakati nyingine zikiimarika.

"Tumekuwa hivi tulivyo na hatuwezi katika siku moja kubadilika kuwa kama Chelsea katika namna ambayo wanasajili wachezaji," alisema Klopp ambaye ni kocha wa zamani wa Borrusia Dortmund.

"Kwa baadhi ya klabu imekuwa tofauti, kwani umiliki wetu pia unatofautiana, nyingine zinamilikiwa na nchi, watu binafsi na nyingine zinamilikiwa na Koo za kitajiri na huo ndio ukweli.

"Tumekuwa klabu ya kitofauti kidogo. Tumefika fainali mbili za Ligi ya Mabingwa Ulaya miaka miwili iliyopita, tukashinda mwaka uliofuata ubingwa wa EPL kwa kutofanya usajili kama klabu nyingine".





# England kurudisha mashabiki viwanjani

**LONDON,** England

WAZIRI Mkuu wa England, Boris Johnson amesema wataupitia upya mkakati wa uwezekano mpya wa kuwaruhusu mashabiki kuingia viwanjani kuanzia Oktoba Mosi, mwaka huu.

Johnson amethibitisha hilo wakati akizungumzia uwezekano wa mashabiki kurudi viwanjani ambapo amesema baadhi ya matukio kutakuwa na idadi maalumu ya kuingia kwa watazamaji 1000 pekee waliokaa katika hali ya mita moja kutoka kwa mwingine.

"Lazima tuje na mpango kazi juu ya kuruhusu idadi kubwa ya mashabiki kwenye viwanja vya michezo baada ya mwezi huu, lakini tunafikiria mashabiki wanaweza kurejea kuanzia Oktoba Mosi," alisema Boris.

Waziri wa Utamaduni, Oliver Downden alisema, "Tunajua mashabiki wana hamu ya kurudi na baadhi ya kazi zinahusiana na matukio hayo, lakini matumaini yapo makubwa kuwa kufikia siku kuu za mwishoni mwa mwaka huu hadhira itakuwa imerudi."

Michezo mikubwa England imekuwa ikiendelea bila uwapo wa mashabiki ambapo FA iliruhusu michezo kuchezwa baada ya kupungua kwa makali ya mlipuko wa virusi vya corona, michezo kama Kombe la FA, Ligi Kuu nchini England, formula 1 pamoja na michezo mingine.

Mapema Jumatano Mkurugenzi wa EPL, Richard Masters alisema: "Ingewezekana mashabiki wangerudi mapema viwanjani kwani kuchelewa kufanya hivyo klabu zitaingia kwenye hasara ya pauni milioni 700 katika msimu wa 2020/21 unaoanza Jumapili hii.

Mwishoni mwa Agosti, mashabiki 2500 waliruhusiwa kuingia uwanjani kuangalia mechi kati ya Chelsea dhidi ya Brighton katika dimba la Amex.

# James aahidi makombe Everton

**LONDON,** England

NYOTA mpya wa Everton, James Rodriguez, anaamini klabu hiyo ipo makini kwenye mambo yake, lakini pia amepanga kuifanya timu kuwa kubwa na kuwania mataji.

James ambaye alikuwa sehemu ya kikosi cha Real Madrid kilichoshinda taji la LaLiga nchini Hispania, msimu uliopita na sasa anaamini watafanya makubwa zaidi akiwa na Everton.

Itakumbukwa mwaka 2014 aliibuka kuwa mfungaji bora wa Kombe la Dunia na amejiunga na Everton kwa ada ya pauni milioni 12 ambapo alifunga mabao 17 kwenye mechi 40 ambazo alicheza chini ya uongozi wa kocha Carlo Ancelotti pale Real Madrid.

Licha ya kushinda mataji tisa, lakini kiwango chake kimekuwa hakieleweki ambapo kilikuwa kinabadilika kila kukicha kama 'homa ya msimu'.

Raia huyo wa Colombia mwenye umri wa miaka 29, anaamini kufanya kazi chini ya kocha Ancelotti, kutamfanya kurejesha makali yake na kushinda mataji ndani ya Everton, kwani uwezo wanao.

"Everton ni klabu inayofanya biashara, kuna watu waliojidhatiti katika viwango vya juu kuifanya timu kufikia makubwa yaani kushinda makombe," alisema James ambaye amewahi kufanya kazi na Ancelotti, akiwa Bayern Munich kwa mkopo.

"Sio jambo ambalo linatokea kwa usiku mmoja, ni mpango wa muda mrefu. Lakini, tumeona saini nzuri na kuna ishara tunakoelekea ni kuzuri maradufu. Inaonekana mataji hayako mbali nasi kama si mwezi ujao, miezi na miaka ijayo".

Everton mpaka sasa wamefanya usajili wa wachezaji watatu kwa jumla ya pauni milioni 53, ambazo zimewaleta katika timu hiyo James Rodriguez, Allan na Abdoulaye Doucoure.






# UNITED SASA YAFIKIA PAZURI NA SANCHO

**MANCHESTER,** England

KLABU ya Manchester United imefikia pazuri katika kukamilisha uhamisho wa winga wa timu ya Taifa ya England na Borrusia Dortmund, Jadon Sancho.

'Mashetani Wekundu' hao, ni kama wameamua kuvunja kibubu cha kukubali mshahara wa mchezaji huyo na ada ya wakala kwa lengo la kukamilisha usajili wa "mtu anayetajwa kuwa tegemeo la usajili dirisha hili kubwa."

Licha ya hatua hizo, lakini bado hakuna makubaliano yoyote ambayo yamefikiwa baina ya Borussia Dortmund na Man United, ambapo Dortmund wanahitaji pauni milioni 120, wakati United wanaonekana kutokuwa tayari kulipa kiasi hicho kuelekea mwishoni mwa dirisha la usajili Oktoba 5.

Baadhi ya ripoti zinadai kuwa huenda Dortmund wakashusha bei ya staa huyo, endapo dirisha la usajili litakaribia kufungwa bila kujitokeza kwa timu zenye uwezo wa kumnunua, ingawa pia pauni milioni 100 zinaweza kukubaliwa.

Wiki iliyopita, Man United walikamilisha usajili wa kiungo mshambuliaji wa timu ya Taifa ya Uholanzi na Ajax, Donny van de Beek kwa dau la pauni milioni 35 na kuwa usajili wa kwanza kwa kocha Ole Gunnar Solskjaer.

# *Lampard: Nimekuja kuipa Chelsea mataji*

**LONDON,** England

KOCHA wa Chelsea, Frank Lampard amesema alijiunga na klabu hiyo kwa ajili ya kushinda mataji na si kung'ang'ania nafasi ya nne kama timu nyingine zinavyofanya.

Kauli hiyo inakuja kipindi ambacho Lampard amesaidiwa na mmiliki wa timu hiyo, Roman Abramovich, ambapo Chelsea ni miongoni mwa timu ambazo zimetumia kiasi kikubwa cha fedha kwenye majira haya ya dirisha kubwa la usajili, pauni milioni 200 zimetumika kuwavuta wachezaji sita.

Klabu hiyo ilikuwa chini ya zuio la Fifa msimu uliopita, ambapo Lampard alilazimika kutumia wahitimu wa akademi yao na kumaliza nafasi ya nne na kufika fainali ya Kombe la FA wakapoteza dhidi ya Arsenal.

Lampard alisema kuingia kwa wachezaji wapya kumeongeza morali kwao na kufanya vizuri zaidi ya msimu uliopita.

"Sikuja hapa kupigania nafasi ya nne au kuwapandisha vijana kutoka timu ya wadogo, nimekuja hapa kushinda kila kitu. Msimu uliopita hatukufanya usajili msimu huu tumefanya hivyo," alisema.

Chelsea wamemsajili kiungo mshambuliaji wa Ujerumani, Kai Havertz ,kwa ada ya pauni milioni 72, lakini wakamchukua pia Mjerumani mwingine Timo Werner kwa pauni milioni 48 na beki wa pembeni wa Leicester City, Ben Chilwell kwa pauni milioni 45.

Hakim Ziyech, Thiago Silva na Malang Sarr ni miongoni mwa majina mapya Stamford Bridge katika msimu unaoanza kesho.



# DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA




# AUBAMEYANG APEWA MIAKA MITATU ARSENAL

## ●●● Mchezaji huyo wa kimataifa wa Gabon alitua Arsenal akitokea Borussia Dortmund...

**LONDON,** England

STRAIKA wa Arsenal, Pierre-Emerick Aubameyang anatarajiwa kusaini mkataba mpya wa miaka mitatu ambao utamfanya kuwa mchezaji anayelipwa fedha nyingi zaidi klabuni hapo.

**Aubameyang ambaye ana umri wa miaka 31, ndiye mchezaji aliyefunga mabao mengi katika kikosi chote cha Arsenal kwa msimu uliopita ambapo alitikisa nyavu mara 29.**

Wawakilishi wa Aubameyang na Arsenal wamekuwa kwenye mazungumzo kwa zaidi ya mwezi mmoja na ripoti zinadai kuwa muafaka wa mazungumzo hayo unakwenda kumpa mkataba wa miaka mitatu ambao utakuwa na mshahara mkubwa zaidi ya ule anaopokea Mesut Ozil wa pauni 350,000 kwa wiki.

Inalezwa kuwa mchezaji huyo amefikia uamuzi wa kubaki baada ya ushawishi mkubwa uliofanywa na baba yake pamoja na kocha wa miamba hiyo, Mikel Arteta.

Nahodha huyo wa Arsenal kwa sasa amebakisha mwaka mmoja kwenye mkataba wake ambapo anachukua pauni 200,000 kwa wiki, jambo lililowaweka Arsenal kitanzini kuamua kati ya kumpa mkataba mpya.

Inter Milan na Barcelona ni kati ya klabu ambazo zinaitamani saini ya mchezaji huyo, lakini mbali ya klabu hizo miamba kadhaa ya soka barani Ulaya imekuwa ikimmezea mate.

Auba ataongeza mkataba huo wa miaka mitatu ambao utamfanya kubaki hapo hadi mwaka 2023, baada ya mazungumzo yaliyofanywa na Raul Sanllehi kabla ya kufika kwa Mkurugenzi wa Ufundi, Edu na mtu wa mwisho kukamilisha dili hilo ni Huss Fahmy ambaye anahusika na masuala ya mikataba ya wachezaji.

Mshahara mpya utamfanya kumpita hadi Willian, aliyesajiliwa kutoka Chelsea, anayelipwa pauni 220,000 kwa wiki.

Mchakato wa kutaka kumbakisha ulianza mara tu baada ya Arteta kuteuliwa kuwa kocha mpya wa kikosi hicho, hiyo ikiwa ni baada ya Arsenal kushindwa kumsainisha mkataba mpya mwaka 2019.

Mchezaji huyo wa kimataifa wa Gabon alitua Arsenal akitokea Borussia Dortmund mwaka 2018.

## ZISIKUPITE

### SAMATTA KUONDOKA VILLA

MSHAMBULIAJI wa kimataifa wa Tanzania, Mbwana Samatta mwenye umri wa miaka 27, ataweza kuondoka Aston Villa ikiwa ni miezi minane tu baada ya kujiunga na klabu hiyo. ***(Mail)***

### CHELSEA YAMKATALIA KANTE

CHELSEA imekataa ofa ya Inter Milan kwa ajili ya kiungo wake aliyetwaa Kombe la Dunia akiwa na Ufaransa, N'Golo Kante mwenye umri wa miaka 29, ofa ambayo inajumuisha kubadilishana na kiungo wa Croatia, Marcelo Brozovic, 27. ***(Guardian)***

### SMALLING KUTUA RASMI ROMA

MLINZI wa Manchester United, Chris Smalling mwenye umri wa miaka 30, hajahudhuria mazoezi wiki hii akikaribia kutua ligi ya Italia, Serie A, kwenye timu ya Roma, kwa uhamisho wa kudumu. ***(Telegraph)***

### WIJNALDUMU ATETA NA KLOPP

KIUNGO wa Liverpool, Georginio Wijnaldum mweye umri wa miaka 29, amefanya mazungumzo yaliyoenda vizuri na kocha Jurgen Klopp kuhusu mustakabali wake klabuni hapo. Mholanzi huyo amebakiza mwaka mmoja kwenye mkataba wake pale Anfield. ***(Sky Sports)***

### ROSE KUONDOKA TOTTENHAM

MLINZI wa England na Tottenham, Danny Rose, 30, anakaribia kutimka Ligi Kuu ya England na kujiunga na kikosi cha Genoa ya Italia. ***(PA, via Team Talk)***

### MARTINEZ ANUKIA MI4 VILLA

GOLIKIPA wa Arsenal, Emiliano Martinez , 28, amekubali mkataba wa miaka minne na Aston Villa, wenye thamani ya pauni 60,000 kwa wiki, wakati huo klabu hizo zikitarajiwa kukubaliana ada ya uhamisho ya zaidi ya pauni milioni 15. ***(Independent)***

### FRED APUZA KUTUA UTURUKI

KIUNGO wa Manchester United na Brazil, Fred mwenye umri wa miaka 27, amepuuza ripoti kwamba anaweza kuondoka msimu huu na kujiunga Galatasaray ya Uturuki. ***(Four Four Two)***

### IVANOVIC KUIBUKIA CHELSEA

KLABU ya West Brom ipo kwenye mazungumzo ya kumnasa mlinzi wa zamani wa Chelsea, Branislav Ivanovic , 36, kwa uhamisho huru baada ya kutemwa na Zenit St Petersburg ya Urusi. ***(Telegraph)***

### MORRISON KUTIMKIA UHOLANZI

KIUNGO wa zamani wa Manchester United, Ravel Morrison, 27, yuko kwenye mazungumzo na klabu za Uholanzi za Vitesse Arnhem na Utrecht baada ya kutemwa na Sheffield United. ***(Mail)***

### WOODBURN KWENDA SPARTA

MSHAMBULIAJI wa Liverpool na Wales, Ben Woodburn, 20, anatarajiwa kujiunga na Sparta Rotterdam ya Uholanzi kwa mkopo wa msimu mzima. ***(Standard)***

### WAMSHINDWA SOUMARE

OFA ya Newcastle ya pauni milioni 32 imekataliwa na Lille kwa ajili ya kumsajili kiungo wa Ufaransa mwenye umri wa miaka 21, Boubakary Soumare. ***(Fabrizio Romano)***

# MAGORI AWATOA HOFU SIMBA UWEKEZAJI WA MO

**Na Adam Fungamwango**

MJUMBE wa Bodi wa Simba, Crescentius Magori amewatoa hofu wanachama na mashabiki wa Simba kuhusu uwekezaji ndani ya Simba kwa kusema uko sahihi na ucheleweshwaji wa kuingizwa kwa fedha kiasi cha Sh. bilioni 20 hauko mikononi mwao, bali kwenye taasisi zingine za kifedha na kiserikali na uhakiki ukishamalizika, kila kitu kitakuwa sawa.

**Akizungumza jijini Dar es Salaam jana, Magori alisema watu wanaohoji bilioni 20 wasitarajie kuwa zikiwekwa basi watagawana, au zitatosha kuiendesha klabu kwa miaka yote, bali zitafanya mipango ya kuiendesha Simba, kutokana na kuwa na mahitaji makubwa mno kwa sasa.**

Mjumbe huyo alisema hayo kufuatia baadhi ya watu kuibuka hivi karibuni na kuhoji uwekezaji ndani ya klabu hiyo, huku wakiuliza ucheleshwaji wa pesa hizo zilizoahidiwa na Mwekezaji Mohamed "Mo" Dewji.

"Kwanza mpaka sasa hakuna mtu ambaye anaweza kubadilisha hiki kilichopo. Ni wanachama na klabu ndiyo waliamua hivi, ndiyo waliobadilisha katiba na ndiyo waliomkubali mwekezaji Dewji, tena kwa kuendesha mchakato wa kumsaka hadi akapatikana," alisema Magori.

Alisema ucheleweshwaji huu unatokana na ugeni wa klabu ya mpira kwenda kwenye uwekezaji, kitu ambacho hakikuwapo huko nyuma kwa klabu nyingi si Tanzania tu, bali Afrika Mashariki.

"Halafu pia kuna watu wanauliza pesa imecheleweshwa au uwekezaji unachelewa kukamilika wakati tuliona hapa nyuma kuna watu walizuia hati ya jengo, sasa watu watawahi vipi wakati kuna watu kazi yao kuzuia tu maendeleo?" Alihoji.

Magori anaamini kuwa baada ya taasisi za kifedha na kiserikali kukamilisha kila tu, kiasi cha Sh. bilioni 20 kitaingizwa, lakini hao hao watu wanaohoji kwa sababu hawana nia nzuri, bado watazua kitu kipya.

Alisema mwaka 2003 wakati Dewji alipojiondoa kuidhamini Simba, kuna baadhi ya watu walijitokeza kuichangia klabu hiyo, lakini hawaongei maneno ya kukatisha tamaa au kuiongelea vibaya klabu, lakini watu wasio na uchungu ndiyo wameonekana zaidi kutoa maneno yasiyofaa.

Kuhusu Ofisa Mtendaji mpya, Barbara Gonzalez, Magori alisema kuwa tangu yeye akiwa Ofisa Mtendaji, mwanadada huyo alikuwa akimsaidia mambo kadhaa, hivyo hakuna ulazima wa kuajiriwa mtendaji mwingine, hivyo alimwambia Mwenyekiti wa Bodi kuwa mwanadada huyo anafaa.

Alisema Barbara ndiye aliyesaidia kuwahi kusajiliwa kwa Chriss Mugalu kutokana na kufanya mambo kwa haraka na uhakika zaidi, jambo ambalo kama si yeye ingeshindikana.



Rais wa TFF, Wallace Karia (kulia) na Mkurugenzi wa Kampuni ya Playmaster, Gevorg Aznauryan, wakibadilishana mikataba jana jijini Dar es Salaam baada ya kampuni hiyo kuingia mkataba wa kudhamini Ligi Daraja la Kwanza na la Pili nchini kwa kipindi cha miaka miwili. **PICHA: JUMANNE JUMA**

## Daraja la Kwanza, zapata mdhamini

**Na Saada Akida**

SHIRIKISHO la Soka Tanzania (TFF), limeingia mkataba wa miaka miwili wenye thamani ya Sh. milioni 240 na Kampuni ya Playmaster kwa ajili ya kusaidia maendeleo ya soka nchini ikiwamo Ligi Daraja la Kwanza na la Pili.

Akizungumza na gazeti hili jijini jana, Rais wa TFF, Wallace Karia alisema wameingia makubaliano na kampuni hiyo ambayo inajishughulisha na Mchezo wa Kubahatisha kwa ajili ya maendeleo ya soka hasa kwa ligi Daraja la Kwanza na Pili ambazo hazina mdhamini.

Alisema baada ya kukaa kwa muda mrefu bila kupata mdhamini wa ligi hizo mbili, sasa wameingia mkataba na kampuni hiyo ili kusaidia timu hizo kuendelea kufanya vizuri.

"Ukizingatia tunatoa timu kutoka Daraja la Kwanza na kwenda kucheza Ligi Kuu, sababu hiyo, tunahitaji kuona ligi hizo mbili zinakuwa na ushindani mkubwa," alisema Karia.

Naye Meneja Mwendashaji wa kampuni hiyo, Mourice Meshack, alisema wameingia makubaliano hayo kwa lengo la kuboresha soka la Tanzania hasa Ligi Daraja la Kwanza na la Pili.

"Tumepanga kufanya makubwa ndani ya soka letu, ukiachilia ligi hizo mbili pia tutajikita na Ligi Kuu," alisema Meshack.

## Riadha Taifa leo kwa Mkapa

**Na Adam Fungamwango**

KATIBU Mkuu wa Wizara ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo, Dk. Hassan Abbas, leo anatarajiwa kuwa mgeni rasmi kwenye ufunguzi wa mashindano ya Riadha Taifa yatakayofanyika Uwanja wa Benjamin Mkapa jijini Dar es Salaam.

Ofisa Habari wa Shirikisho la Riadha nchini Tanzania, Tulo Chambo, alisema jijini jana kuwa, michuano hiyo itafunguliwa leo na kumalizika kesho Jumapili ambapo itafungwa na Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam, Aboubakar Kunenge.

"Tayari mikoa imeshaanza kuwasili. Mikoa yote ya Zanzibar imeshawasili, Kilimanjaro, Arusha, Kigoma na mingine iko njiani," alisema Tulo.

Hata hivyo, alisema mikoa mitatu ya Rukwa, Katavi na Lindi itakosekana kutokana na kutothibitisha kushiriki michuano hiyo ya kila mwaka.

Alisema lengo la mashindano hayo ni wanariadha kuonyesha vipaji vyao na watakaofanya vizuri wataingizwa kwenye rekodi ya Riadha Taifa na kunufaika kwa kushiriki michuano mbalimbali nchini na nje ya nchi.

Ofisa Habari huyo alisema kuwa zawadi kwenye michuano hiyo si fedha, bali ni medali, ambapo washindi wa kwanza watapata medali za dhahabu, medani za fedha kwa washindi wa pili na wale watakaokuwa wa tatu watazawadiwa medali za shaba.

# *Kipenga Ligi Kuu Z'bar chapulizwa*

**Na Hawa Abdallah,** ZANZIBAR

KIPENGA cha kuanza kwa Ligi Kuu Zanzibar kimepulizwa rasmi baada ya Shirikisho la Soka visiwani hapa (ZFF), kutangaza kalenda yake ya matukio mbalimbali kwa msimu mpya wa 2020/2021.

Katika kalenda hiyo, imeonyesha Ligi Kuu Zanzibar kwa msimu huu wa 2020/21 unatarajiwa kuanza Novemba 7, mwaka huu ambapo Novemba Mosi utapigwa mchezo wa Ngao ya Jamii.

Ligi Kuu Zanzibar msimu huu itashirikisha jumla ya timu 12, huku Ligi Daraja la Kwanza Kanda ya Unguja ikiwa na timu 12 wakati Kanda ya Pemba zitakuwa timu 18, lakini pia kutakuwa na Ligi Kuu ya Wanawake pamoja na Ligi ya Vijana.

Aidha, kalenda hiyo inaonyesha kuwa Oktoba 5, mwaka huu kutakuwa na semina elekezi kwa makatibu wa klabu na wenyeviti itakayohusu kanuni ya mashindano kwa msimu huu, huku mtihani wa kujipima utimamu wa mwili kwa waamuzi (Copa test) ukitarajiwa kufanyika Oktoba 25.

Akizungumza na gazeti hili jana, Mkurugenzi wa Mahindano wa ZFF, Ali Mohammed Ameir, alisema klabu zinatakiwa kufuata kalenda hiyo ili kuepuka usumbufu wa kuchelewa kufanya taratibu zote ikiwamo kipindi hiki cha usajili.

Alisema baadhi ya klabu zinachelewa makusudi kufanya usajili hadi tarehe za mwisho ambapo husababisha usumbufu ikiwamo kuchelewa kurejesha fomu kwa wakati uliowekwa licha ya ZFF kuchukua hatua kwa mujibu wa kanuni ya mashindano.

"Ni muhimu klabu kufuata Kalenda ya ZFF, kulingana na matukio yote yaliyowekwa yanayohusu mashindano, hii itasaidia kwenda na muda, inabidi sote kwa pamoja tubadilike katika kukimbizana na muda kutokana na msimu uliopita kuvurugika kulikosababishwa na mlipuko wa virusi vya corona, hivyo msimu huu tujitahidi kufanya shughuli zetu zote kwa wakati," alisema.

Ligi Kuu Zanzibar msimu huu itashirikisha timu za MLandege FC, Malindi SC, Chuoni FC, KVZ SC, KMKM SC, Zimamoto SC, Kipanga FC, Polisi FC, JKU SC, Mafunzo SC, Black Sailor na timu moja kutoka Kanda ya Pemba.

# Michezo

Jumamosi Septemba 12, 2020

Nipashe




Aubameyang apewa miaka 3 Arsenal UKURASA 22

**UZI MPYA...**



Makamu Mwenyekiti wa Yanga, Frederick Mwakalebela (kushoto) akimpongeza Mkurugenzi wa Uwekezaji wa Kampuni ya GSM, Mhandisi Heris Said, wakati wa kutambulisha jezi mpya za klabu hiyo katika uzinduzi uliofanyika jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: JUMANNE JUMA**

## Jezi mpya Yanga zaibua shangwe

**Na Saada Akida**

JEZI Mpya za Klabu ya Yanga zimekuwa gumzo baada ya kuteka hisia za mashabiki wengi waliojitokeza katika makao makuu ya timu hiyo yenye maskani yake mitaa ya Twiga na Jangwani jijini Dar es Salaam.

Jezi ya nyumbani imeonekana kuwa kivutio zaidi kwa mashabiki wao na kuibua shangwe kutokana uzuri na ubora wake, wakati zikitambulishwa rasmi jana.

Akizungumza na gazeti hili jijini jana, Mkurugenzi Uwekezaji wa Yanga, Mhandisi Hersi Said, alisema jezi za msimu huu zina ubora na zimetengenezwa kuendana na utamaduni wa Kitanzania kwa kufuata rangi ambazo zipo katika bendera ya Taifa, hivyo zinaendana na uhalisia wa timu ya Wananchi.

"Tumezindua jezi mbili ya nyumbani na ugenini, mbadala ya tatu tunataraji kuiweka hewani hivi karibuni, katika utengenezaji wa jezi za msimu huu zinaendana na utamaduni wa Afrika hasa kwa kuzingatia nchi yetu ikiwamo rangi," alisema Hersi.

Makamu Mwenyekiti wa Yanga, Fredrick Mwakalebela, alisema; "Tumechelewa kuzindua jezi kwa sababu ya kutokea kwa janga na corona, ukizingatia kuna mataifa mengi bado mipaka yao haijafunguliwa, ila sasa tayari tumezipata tunaomba mashabiki wanunue jezi halisia na kuachana na feki."

Kwa upande wa Mkurugenzi wa SpotiPesa Tanzania ambao ni wadhamini wa klabu hiyo, Abbas Tarimba amezitaka mamlaka ya vyombo vya usalama kuwachukulia hatua kali wanaotengeneza na kuuza jezi feki.

# MIQUISSONE, MUGALU WAINOGESHA SIMBA

**Na Somoe Ng'itu,** MOROGORO

### Sven awatahadharisha wakati wakiivaa Mtibwa leo huku akiutaja uwanja...

MABINGWA watetezi wa Ligi Kuu Bara, watashuka katika dimba la Jamhuri mjini Morogoro leo kuivaa Mtibwa Sugar katika mechi ya raundi ya pili ya ligi hiyo msimu huu huku wakijivunia kikosi kipana kwa wachezaji wote kuwa fiti kucheza mechi hiyo inayotarajiwa kuwa ngumu kwa pande zote.

**Baada ya kuwakosa mshambuliaji wake mpya, Chris Mugalu, kiungo mshambuliaji Luis Miquissone, kiungo wa kati Gerson Fraga na beki wa kati Pascal Wawa kwenye mechi ya ufunguzi wa ligi hiyo dhidi ya Ihefu FC wakati wakishinda 2-1 kwenye Uwanja wa Sokoine, wachezaji hao wameelezwa kuwa tayari kwa mchezo huo wa leo.**

Kiu ya mashabiki wa Simba ni kuona Miquissone akicheza winga ya kulia huku Mghana Bernard Morrison akitawala winga ya kushoto na Mugalu akisimama kama mshambuliaji wa kati.

Katika mechi ya awali, wachezaji hao waliachwa jijini Dar es Salaam wakiendelea na progamu maalum kutokana na kuchelewa kujiunga kambini na wenzao, lakini Meneja wa Simba, Patrick Rweyemamu, amesema kwa sasa wapo fiti vya kutosha kuweza kucheza mechi hiyo.

"Tumekuja Morogoro na wachezaji wote 28 waliosajiliwa, Miquissone, Wawa na Mugalu wote wapo fiti ni jukumu la kocha tu kuamua nani wa kuanza," alisema Rweyemamu.

Alisema mechi hiyo itakuwa ngumu, lakini lengo lao ni kupata pointi tatu na hawataingia uwanjani wakitazama matokeo waliyoyapata msimu uliopita katika uwanja huo.

Msimu uliopita Simba ilivuna pointi zote sita dhidi ya Mtibwa ambapo mechi ya mzunguko wa kwanza katika Uwanja wa Mkapa ilishinda mabao 2-1 kabla ya kushuka dimba la Jamhuri mjini Morogoro ambapo John Bocco, Hassan Dilunga na Meddie Kagere wakaiongoza kushinda 3-0.

Kocha Mkuu wa Simba, Mbelgiji Sven Vandenbroeck, yeye amesema Uwanja wa Jamhuri eneo la kuchezea (pitch) si nzuri na kwamba ni afadhali ule wa Sokoine, hivyo amewataka wachezaji wake kulifahamu hilo mapema wakati wakishuka dimbani leo kuivaa Mtibwa.

"Katika mchezo uliopita dhidi ya Ihefu mara nyingi ilibidi tutumie mipira mirefu kwa kuwa hatukuweza kucheza soka letu la pasi fupi fupi sababu ya uwanja kutokuwa mzuri, lakini huu wa Jamhuri nao hauridhishi, tumefanya mazoezi na kugundua hauna tofauti na ule wa Sokoine, hivyo inabidi wachezaji wauzoee mapema.

"Kwa ujumla wachezaji wapo kwenye hali nzuri, japo eneo la kuchezea sio nzuri, lakini tumejipanga kukabiliana na hali yoyote," alisema Sven ambaye amerithi mikoba ya Mbelgiji mwenzake, Patrick Aussems.

Kuhusu mchezo huo, alisema mara zote Simba inapokutana na Mtibwa Sugar ushindani unakuwa mkubwa ingawa msimu uliopita walipata ushindi katika mechi zote mbili za ligi.

Mechi nyingine zitakazopigwa leo itakuwa ni JKT Tanzania dhidi ya Dodoma Jiji wakati KMC FC ikiialika Tanzania Prisons katika Uwanja wa Uhuru jijini Dar es Salaam.

Ligi hiyo itaendelea kesho kwa Yanga kuikaribisha Mbeya City kwenye Uwanja wa Mkapa huku Ihefu FC ikiwa mwenyeji wa Ruvu Shooting katika dimba la Sokoine jijini Mbeya na Biashara United ikiialika Mwadui FC kwenye Uwanja wa Kumbukumbu ya Karume mjini Musoma.

9 770856 541002 >

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042